**Rufani** ya kina Mdee bado kizungumkuti

UKURASA 3



**Daktari** Bingwa asimulia kesi mauaji ya Mawazo

UKURASA 4



**Karembeu amtaka Mbappe kuamua**

UKURASA 20


# Nipashe

Jumatatu Desemba 14, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580429

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# MAUAJI YA KUTISHA

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**ACT KUPELEKA WABUNGE KUAPA**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimekubali wabunge wake walioshinda nafasi...

UKURASA WA 4

**SITA WA FAMILIA MOJA WAHUKUMIWA KUNYONGWA**

WATU saba wakiwamo sita wa familia moja wilayani Tarime na Serengeti...


## Utashi kisiasa ulivyoongeza faru wapya 29 mwaka 1



UKURASA 3



Wahitimu wa Mahafali ya 18 wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Kampasi za Singida, Mwanza na Kigoma, wakirusha kofia zao juu ikiwa ni ishara ya kuonyesha furaha zao kwenye mahafali hayo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Singida. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Rungu laja 'Day Care' za mitaani

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA KUCHAGUA M'KITI JANUARI** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Corona yapaisha bei ya mbolea, wakulima walia

**Na Thobias Mwanakatwe**

BEI ya mbolea imepanda maradufu ambapo baadhi ya mikoa inauzwa kati ya Sh.68,000 hadi 90,000 kwa mfuko, hali ambayo imezua taharuki na malalamiko mengi kutoka kwa wakulima.

Kupanda bei kwa mbolea hizo kuliibuliwa juzi usiku na mkulima mmoja kutoka Tunduma mkoani Songwe, ambaye alipiga simu kwenye kipindi cha Papo kwa Papo kinachorushwa na runinga ya Chanel Ten ambacho kinaendeshwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Taifa, Humprey Polepole, kusikiliza kero za kuzipatia ufumbuzi papohapo. Kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika mbolea ilikuwa inauzwa bei ya chini, lakini baada ya uchaguzi bei imeongezeka kutoka Sh. 54,000 hadi kufikia 68,000 kwa mbolea aina ya DAP. Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, akijibu swali hilo, alithibitisha mbolea kupanda bei nchini ambapo baadhi ya mikoa inauzwa hadi Sh. 90,000 kwa mfuko.

"Katika kipindi kifupi kumekuwa na ongezeko la bei ya mboleo tuliyonayo ambapo ongezeko hilo ni kati ya Sh. 5,000 hadi 11,000,'' alisema.

Kusaya alisema kuongezeka kwa bei ya mbolea kumetokana na ugonjwa wa Corona ambao umeziathiri nchi zinazozalisha mbolea, hivyo kusimama uzalishaji huku uhitaji kuwa mkubwa. "Juzi nilikwenda Kagera, mbolea ya UREA inauzwa hadi 90,000, Sirali nako inauzwa bei juu,'' alisema.

Alisema mahitaji ya mbolea nchini kwa mwaka ni tani 638,000 ambapo mboleo yote tunaitegemea kutoka nje ya nchi. "Hapa nchini hatuna kiwanda kikubwa ambacho kinaweza kutupatia tani 638,000, kiwanda pekee tulichonacho ambacho ni cha Minjingu kilichopo mkoani Manyara uwezo wake kikijitahidi sana hakiwezi hata kufikia tani 150,000 kwa mwaka,'' alisema.

Kusaya alisema ongezeko hilo la bei limekuwapo na limejitokeza zaidi baada ya India kutangaza kuhitaji mbolea zaidi ya tani milioni 1.2 ambayo ni mahitaji makubwa ukilinganisha na uzalishaji uliopo.

Alisema kutokana na tatizo hilo, serikali imejitahidi kuwahamasisha na kuwasihi wananchi waanze kutumia mbolea za asili kama samadi.

Aliongeza kuwa pia serikali inawahamasisha wafanyabiashara kujitokeza kuwekeza kwa kujenga viwanda vya mbolea .

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati kipindi kikiendelea, alituma ujumbe mfupi kwenye simu ya Polepole na kutoa maelekezo kwa mkurugenzi kuanzia leo atoe matangazo kwenye vyombo vya habari kuhusu bei elekezi ya mbolea.

Bashe alisema atakayebainika kuuza zaidi ya bei elekezi ya serikali, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

# Mauaji ya kutisha

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Festo Venance (38), kwa tuhuma za kuwaua watu wawili akiwamo mtoto mwenye umri wa miaka mitatu na kumjeruhi mmoja katika Kijiji cha Kumzuza, wilayani Ngara.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kutumia kitu chenye ncha kali kuua watu hao na kujeruhi, huku mbuzi watano wanaomilikiwa na aliyejeruhiwa wakichinjwa.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo na kuwataja waliouawa kuwa ni Magreth Jacob (33), ambaye alikuwa hawara wa mtuhumiwa, na mtoto Jonam Niyonzima (3).

Alimtaja aliyejeruhiwa kuwa ni Penina Joseph (40), ambaye amelazwa katika Hospitali ya Murgwanza, wilayani humo na hali yake kuwa mbaya kutokana na kuvuja damu nyingi.

"Mtoto Jonam (aliyeuawa) ni wa kaka yake Penina (majeruhi), Imani Joseph, ambaye ni Mwenyekiti wa kitongoji cha Mukishusha na kwamba wakati wa tukio mtoto huyo alikuwa na shangazi yake, baada ya mama mzazi, Rebeca Mushengezi (38), kumuomba wifi yake aondoke naye akalale kwake hadi asubuhi watakapokutana wakienda katika vibarua," alisema.

Kamanda Malimi alisema usiku wa kuamkia siku ya tukio Desemba 10, mwaka huu, wahusika wote walionekana wakiwa baa inayouza pombe za kienyeji inayomilikiwa na Juma Ndahuro na baadaye waliamua kuondoka na kumwacha Rebeca akiendelea kunywa pombe, kabla ya kupata taarifa za mtoto wake kuuawa.

"Usiku saa kumi, mtuhumiwa alikwenda nyumbani kwa Imani na kumwambia mdogo wako (Penina) anauawa ...baba huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mukishusha lilipotokea tukio hilo, hakuamka hadi asubuhi alipopata taarifa za mauaji hayo ikiwamo kukuta mdogo wake ni majeruhi vibaya," alisema.

Kamanda alisema kuwa mtuhumiwa pamoja na kuwa na familia ya mke na watoto, alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na Magreth yaliyoanza baada ya kufiwa na mume wake.

"Ilipofika asubuhi miili ya watu hao iligunduliwa na wapita njia, na mtuhumiwa hakuonekana tena katika eneo hilo hadi alipokamatwa na wananchi akiwa mafichoni akijiandaa kutoroka, ambao walimfikisha polisi," alisema Kamanda Malimi.

Alisema chanzo cha mauaji hayo bado hakijafahamika na mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa. Hata hivyo, alifafanua kuwa mtuhumiwa hajakiri kuhusika ingawa kuna baadhi ya mazingira yanaonyesha kuhusika kwake, ikiwamo nguo alizokuwa amevaa kukutwa na damu.

"Anayeweza kutueleza kilichotokea ni majeruhi Penina ambaye alishuhudia, lakini hali yake siyo nzuri bado hajaweza kuzungumza, anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Murgwanza," alisema Kamanda huyo.

Kadhalika, Kamanda Malimi alisema katika tukio hilo pia, mbuzi watano mali ya Penina walishambuliwa kwa kukatwa kwa kitu chenye ncha kali, hali inayothibitisha kuwa mtuhumiwa huyo wa mauaji alikwenda nyumbani kwa mama huyo na kuua mifugo hiyo.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kujua chanzo cha tukio hilo ikiwamo kubaini kama watu wengine walihusika na mauaji hayo.



Balozi wa China nchini, Wang Ke (kushoto), akipokea nakala ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kutoka kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk Bashiru Ally, mara baada ya mazungumzo yao yaliyofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: VALENTINE OFORO**

# Rungu laja Day Care' za vichochoroni

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

SERIKALI imetoa siku 14 kwa wamiliki wa vituo vya malezi vya watoto na (Day Care), kurekebisha kasoro ili watoto hao walelewe katika mazingira sahihi na kwa kujibu wa sheria.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, alitoa agizo hilo jijini Arusha baada ya kutembelea baadhi ya vituo na kubaini kutozingatia masharti ya utoaji wa huduma kwa watoto kama ilivyoainishwa kwenye sheria na miongozo.

"Eneo hili (kwenye kituo kimojawapo), halikidhi vigezo na mazingira ya kuwa kituo cha malezi ya watoto mchana, kwa hiyo nawapa wiki mbili mrekebishe upungufu wote, mtafute eneo jingine, maofisa ustawi waje kufanya ukaguzi baada ya siku 14, kama hamjakidhi tutakifunga," alisema Dk. Jingu.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, huduma ya malezi kwa watoto inapaswa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwamo vyumba vya madarasa, viwanja vya michezo na wahudumu wa kutosha na wenye sifa.

Alisema wizara imepanga kufanya operesheni maalum kwenye vituo hivyo nchi nzima ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009.

Nao, baadhi ya wasimamizi wa vituo vilivyokaguliwa, wamekiri vituo hivyo kuendeshwa kinyume cha utaratibu ikiwamo kutokuwa na usajili pamoja na mazingira yasiyofaa kwa malezi ya watoto.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu amewataka Maofisa Ustawi wa Jamii jijini Arusha kukagua vituo vya malezi ya watoto mara kwa mara ili kubaini kasoro na kuzitafutia ufumbuzi.

Dk. Jingu alisema ukaguzi aliofanya katika baadhi ya vituo hivyo vya kuelelea watoto, umethibitisha maofisa hao hawatembelei vituo.

"Kuna changamoto ya kutofanya ukaguzi wa makao na malezi ya watoto, matokeo yake vituo hivyo haviendeshwi kulingana na utaratibu na ukaguzi wetu umethibitisha hivyo, tufanye ukaguzi mara kwa mara kwani tusipofanya hivyo hatutajua nini kinafanyika huko," alisisitiza.

Wiki iliyopita baadhi ya vituo vya kulelea watoto katika Manispaa ya Kinondoni vilifungiwa kutoa huduma ili kufanya marekebisho na kuzingatia sheria ya uanzishaji wa vituo hivyo.

# Utashi wa kisiasa ulivyoongeza faru wapya 29 mwaka mmoja

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limesema kuwa utashi wa kisiasa umesaidia wanyamapori waliokuwa mbioni kutoweka kuzaliana na kurejesha idadi yake.

Kutokana na jitihada hizo faru 29 wameongezeka tangu mwaka 2018 hadi sasa, huku mpango wa kuongeza wanyama hao ukiwa na lengo la kufikisha idadi ya 205 kutoka mwaka 2019 hadi 2023.

Mratibu wa Faru nchini wa TANAPA, Philbert Ngoti, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, akiwasilisha mada ya mpango wa uhifadhi wa wanyama waliohatarini kutoweka, wakati wa mkutano na wahariri na waandishi wa habari waandamizi wanaoandika habari za uhifadhi na utalii.

Alisema asilimia 90 ya faru walipotea duniani na kwamba Tanzania miaka ya 1970 walikuwa 10,000 ikiwa nchi yenye faru wengi, ambao walipungua hadi kufika 15 miaka ya 90 kutokana na ujangili.

"Kuanzia Machi mwaka huu, kulikuwa na faru 190, katika Hifadhi ya Taifa Mkomanzi, Great Serengeti Ecosystm inayobeba Hifadhi ya Taifa Serengeti, Mamlaka ya Hifadhi eneo la Ngorongoro, mapori ya Ikorongo, Maswa na Hifadhi ya Taifa ya Masai Mara nchini Kenya," alisema.

Alisema kwa mwaka huu hakuna faru aliyepigwa, na kwamba mwaka jana Faru Fausta alikufa kwa ugonjwa, huku kukiwa na mpango wa kupeleka faru katika Hifadhi ya Taifa Buringi Chato na Hifadhi ya Taifa Arusha.

Ngoti alisema kuongezeka kwa faru kumetokana na jitihada za taasisi kama TANAPA na zilizopo katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Mkomazi, Arusha na Buringi Chato, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Ngorongoro na Mamlaka ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI).

Mratibu huyo alisema faru hao wanalindwa kwa kifaa maalum cha kufuatilia mienendo yao na taarifa kupokelewa kwenye vituo mbalimbali kwa teknolojia ya kisasa.

"Pembe hizi huuzwa nchini China na Vietnam ambako inatengeneza dawa za kienyeji ambazo huaminiwa zinatibu homa, kupooza, saratani na nguvu za kiume. Vietnam mtu kuwa na jambia au kifaa kilichotengnezwa kwa pembe ya ndovu ni ufahari mkubwa, ndiyo maana hutoa fedha nyingi ili kupata kiungo hicho," alifafanua.

"Kwa sasa ujangili umechangia kupungua, kulikuwa na vigogo wa ndani ya serikali walishirikiana na watu wa nje kuangamiza wanyama hawa ila kwa sasa mkakati uliopo ni kusafisha ndani na ndiyo maana tumeleta jeshi la uhifadhi na misitu," alibainisha.

Naye, Kamishna Msaidizi, Godwell Meing'ataki, alisema utayari wa kisiasa uliopo sasa umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ujangili kwa kuwa miaka ya nyuma wahifadhi walijikuta kwenye matatizo mkubwa walipotaka kuchukua hatua.



Moja ya majengo ya hospitali mpya ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, ambayo inaendelea kujengwa, kwa lengo la kupanua huduma za afya wilayani humo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Rufani ya wabunge wa CHADEMA kizungumkuti

**Na Elizabeth Zaya**

RUFANI iliyotajwa kwamba ingekatwa na wabunge 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA), wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA), Halima Mdee bado ni 'kizungumkuti'.

Desemba Mosi, mwaka huu wakizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, wabunge hao, walidai kwamba wangekata rufani ya kuvuliwa uanachama kwa Baraza Kuu la chama baada ya kushauriana na wanasheria wao.

Wakiwa katika mkutano huo na waandishi wa habari, walidai kukata rufani hiyo, ikiwa ni siku moja baada ya kupewa barua rasmi ya kufukuzwa uanachama wao na Kamati Kuu ya CHADEMA.

Mdee alisema ndani ya siku 30, baada ya kutafakari na kushauriana na wanasheria wao watakuwa wamekata rufani hiyo kwa Baraza Kuu la chama hicho huku akidai kwamba kwa kipindi hicho chote ambacho watakuwa wakisubiri uamuzi wa rufani wataendelea kuwa wanachama wa hiari na ving`ang`anizi kutokana na mapenzi waliyonayo kwa chama chao.

"Tumekuja hapa tunasema tunaenda kukata rufani Baraza Kuu, sasa kisheria siwezi kujadili hapa nje content ya kile ambacho tutakwenda kujadili na mamlaka za juu ya chama," alisema .

Desemba 3, akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, alisema kwamba kwa mujibu wa Katiba ya chama chao, wanatakiwa kukata rufani ndani ya siku 30 tangu kuvuliwa uanachama ambapo mpaka tarehe hiyo walikuwa hawajakata rufani hiyo.

"Mpaka sasa hatujapokea rufani yoyote kutoka kwa waliokuwa wanachama wetu 19 waliofukuzwa, lakini kama Katiba yetu inavyosema, bado wana muda wa kufanya hivyo, kwa hiyo bado wana muda wa kujipanga.Sisi tunawasubiri na tuko tayari kuwasikiliza,"alisema Mrema.

Jana Nipashe lilipotaka kufahamu kama endapo chama hicho tayari kimepokea barua ya rufani hiyo, hakikujibiwa ndiyo wala hapana.

"Siko ofisini, ngoja niulize kwanza ofisini, labda huenda walipeleka jana, nikipata majibu nitakuambia,"alijibu Mrema alipoulizwa na mwandishi wa gazeti hili.

Baada ya kupigiwa baadae, Mrema hakupokea simu hadi tunakwenda mitamboni.

Kwa mujibu wa Mdee, tangu Desemba mosi walipopata rasmi barua ya kuvuliwa uanachama mpaka sasa ni siku 15. Kwa mujibu wa Katiba ya CHADEMA bado wana siku 15 za kuwasilisha rufani.

# ACT kupeleka wabunge kuapa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimekubali wabunge wake walioshinda nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, upande wa Zanzibar kwenda bungeni kuapa.

Kauli hiyo ya ACT-Wazalendo inakuja siku chache baada ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, kukitaka chama hicho kuwapeleka wabunge hao bungeni kuapa ili wapangiwe kazi za kufanya.

Akizungumza na Nipashe jana, Naibu Katibu, Uenezi, Habari na Mahusiano kwa Umma wa chama hicho, Janeth Rithe, alisema wabunge hao watakwenda bungeni kuapa.

"Wabunge wetu watakwenda bungeni kuapa, sijui ni lini lakini watakwenda," alisema Rithe.

Akizungumza hivi karibuni, Ndugai alisema hakuna sababu kwa wabunge wa chama hicho kuendelelea kuzurula mtaani kama waliomba kuwatumikia wananchi wao.

"Nitoe wito kwa wabunge wengine wowote wale, nafikiri kumbukumbu zangu zinanionyesha kwamba tuna wabunge watatu wa ACT-Wazalendo ambao bado hawajaapa,"alisema Spika Ndugai baada ya kumuapisha mbunge mteule na Naibu Waziri wa Madini, Shukran Manya hivi karibuni.

"Ningeomba kutoa wito na wenyewe wakiwa tayari kuitumikia nchi yao, kama kweli waliomba ubunge kutumikia wananchi, hawana sababu ya kuendelea kuzurula huko waliko, watoe taarifa kwa Spika haraka tuwapangie ili wapate kiapo wafanye kazi ya mbunge kama ambavyo wananchi waliwaamini."

Tayari ACT-Wazalendo imeridhia kushiriki katika kuunda serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar kama ambavyo Katiba inataka.

Uamuzi wa chama hicho kukubali kujenga umoja huo wa kitaifa mwezi mmoja tangu kuundwa kwa Serikali ya Rais Hussein Mwinyi.

Kwa mujibu wa ACT-Wazalendo, uamuzi huo ulifikiwa baada ya majadiliano ya kina ya vikao vya ndani vya chama hicho pamoja na ushirikishwaji wa wananchi ambao inadaiwa wengi waliuridhia.

Miongoni mwa misimamo ambayo chama hicho kilitoa baada ya kukubali kujenga umoja huo ni pamoja na kutaka kufanyika kwa uchunguzi wa kina wa matukio yaliyodaiwa na chama hicho kuwa ni ya uvunjifu wa amani yaliyotokea kabla na baada ya uchaguzi wa Zanzibar na kuchukua hatua, kufanya mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi Zanzibar na kufanya mabadiliko ya uendeshaji wa Idara maalum za Serikali.



Wakazi wa mjini Songea waliojitokeza stendi ya mabasi mjini humo kushuhudia makabidhiano ya gari aina ya Renault KWID kutoka Vodacom kwenda kwa mshindi wa bahati nasibu ya promosheni ya Vodacom Shangwe Shangwena, Gloria Kamanga (hayupo pichani ), ambaye ni mjasiriamali mdogo katika soko la Manzese mjini Songea, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Daktari bingwa asimulia kesi mauaji ya Mawazo

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeendelea kumsikiliza shahidi namba 12 katika kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Geita na mgombea Ubunge Jimbo la Busanda, Alphonce Mawazo kupitia chama hicho.

Shahidi huyo ni Kaima Jackson (59) kutoka upande wa Jamhuri, ambaye ni Daktari bingwa wa Magonjwa ya binadamu kutoka Hospitali ya Bugando ambaye ndiye aliyefanya uchunguzi wa mwili wa Mawazo.

Kesi hiyo inawakabili washtakiwa watano.

Shahidi huyo akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Hezron Mwasimba, alidai kuwa Novemba 16, mwaka 2015 kuanzia saa sita na nusu mchana alifanya uchunguzi wa mwili wa Mawazo akiwa mbele ya askari polisi wawili wa mkoa wa Geita pamoja na ndugu wa marehemu wanne.

Shahidi huyo alidai kuwa kutokana na uchunguzi ilibainika kuwa, marehemu alipatwa na mshituko uliosababishwa na kupungukiwa na damu kwa sababu ya majeraha mbalimbali yaliyokuwa kwenye kichwa yaliyotokana na kupigwa na kitu chenye ncha kali na ncha butu.

"Mwili ambao nilichunguza mwenyewe ni wa marehemu Alphonce Mawazo kwa nje kulikuwa na majeraha kwenye miguu na mikononi, sehemu za miguuni na mikononi ni kimo cha setimita moja mbele ya magoti upande wa nje wa mikono, majeraha ya miguuni yalikuwa mchanganyiko na kuvia kwa damu ndani na majeraha mengine ngozi ilikuwa imekatwa, na mikononi pia palikuwa na majeraha mbalimbali mchanganyiko na silaha iliyotumika ni ncha butu, na majeraha mengine silaha iliyotumika ilikuwa yenye ncha kali,"alidai shahidi huyo.

"Kichwa kilikuwa kimefungwa bandeji na nilimaliza uchunguzi wa mwili wa marehemu Mawazo saa saba mchana kutoa ripoti katika fomu namba 275.

Shahidi huyo aliendelea kueleza mahakama kuwa, mambo mengine kwa nje mwili wa marehemu Mawazo ulikuwa haujaoza na bandeji zote zilikuwa na damu.

Alidai kwamba baada ya kufungua bandeji kwenye kichwa waliona nyuzi zilizokuwa zimeshona majeraha manne na kwenye magoti kulikuwa na majeraha madogo na urefu wake ulikuwa setimita moja.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya kutoa bandeji kwenye kichwa, sehemu ya jeraha kubwa lilikuwa na setimita sita na badaye baada ya kufungua fuvu la kichwa walikuta ubongo umechanganyikana na damu, huku sehemu ya kushoto kukiwa kumejaa damu ndani ya ubongo.

Alidai kwamba sehemu nyingine zote zilikuwa kawaida ikiwamo kwenye kiuno, mgongo, shingo, kifua, tumbo na sehemu za siri.

Aidha, upande wa utetezi wa washtakiwa ukiongozwa na mawakili wa kujitengemea watano ambao ni Yisambi Siwale, Flora Enosy, Laurent Bugoti, Abel Sizya na Paul Hombo walimuuliza maswali shahidi huyo wa upande wa Jamhuri kama ifuatavyo:-

**Wakili:** Nyuzi zilizokuwa zimeshonwa kwenye jeraha kubwa zilikuwa ngapi?

**Shahidi:** Nyuzi zilikuwa 4.

**Wakili:** Marehemu alitokea wapi?

**Shahidi:** Alitokea Hospitali ya Wilaya Geita.

**Wakili:** Taarifa za maiti zilipatikana kwa ndugu wa marehemu au kwenye faili alilokuwa akitibiwa?

**Shahidi:** Kwa ndugu wa marehemu.

**Wakili:** Oda ya uchunguzi wa mwili wa marehemu Mawazo ilitoka kwa nani?

**Shahidi:** Oda ya uchunguzi wa mwili wa marehemu Mawazo ilitoka Jeshi la Polisi Geita.

**Wakili:** Kwa uchunguzi wako marehemu Mawazo alikufa lini?

**Shahidi:** Si zaidi ya saa 48.

**Wakili:** Kwenye uchunguzi wako uliweza kuchukuwa damu ikapimwa ili kuona kama kuna ugonjwa?

**Shahidi:** Hapana.

Wakili: Una uzoefu gani kwenye uchunguzi wa mili ya marehemu?

**Shahidi:** Nina uzoefu wa miaka 20.

Baada ya Mawakili wa kujitegemea kumaliza kuuliza maswali shahidi upande wa Jamhuri. Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Javelin Rugaihuruza nao pia uliendelea kumuuliza maswali shahidi wao kama ifuatavyo:-

**Wakili:** Kifo cha marehemu Mawazo kilitokana na pombe?

**Shahidi:** Majeraha ya marehemu Mawazo hayakuhusiana na pombe.

**Wakili:** Ni jeraha lipi ambalo lilisababisha kifo cha Mawazo?

**Shahidi:** Majeraha ya kichwani ndiyo yaliyosababisha kifo cha Alphonce Mawazo.

**Wakili:** Majeraha ya miguuni na mikononi yalisababishwa na kitu gani?

**Shahidi:** Majeraha ya miguuni na mikononi yalisababishwa na kitu chenye ncha kali na butu.

Tayari mashahidi 12 wametoa ushahidi wao na vielelezo saba, kwa upande wa Jamhuri na unatarajia kupeleka mashahidi hapo mahakamani zaidi ya 20 na vielelezo nane.

Naibu Msajiri Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi Mwenye Mamlaka ya Ziada, Frank Mahimbali aliahirisha kesi hiyo hadi leo kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliyobakia.

Washtakiwa wote walipelekwa mahabusu kwa sababu kesi inayo wakabili ya mauaji haina dhamana

Akisoma hati ya mashtaka Msaidizi wa Kumbukumbu Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Martina Nelei alidai hapo mahakamani kuwa Novemba 14 mwaka 2015 katika Kijiji cha Rudete Mkoa wa Geita washtakiwa wote kwa pamoja wanadaiwa kumuua Alphonce Mawazo, kitendo ambacho ni kinyume cha kifungu 196 na 197 cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Wanaoshtakiwa katika kesi hiyo ni Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45), Habibu Feruzi (34) na Kululinda Bwire (31) wote kwa pamoja ni wakazi wa Katoro mkoani Geita.

## Sita wa familia moja wahukumiwa kunyongwa

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU saba wakiwamo sita wa familia moja wilayani Tarime na Serengeti, mkoani Mara waliokuwa na kesi mbili za mauaji ya watu watatu, wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kuwaua Zabron Mokono, Nyaimwa Matiko na Mwita Waryoba kwa kuwakata mapanga, huku Mwita akitenganishwa kichwa na kiwiliwili na mwili wake kutupwa porini na ndugu zake.

Waliohukumiwa ni Khanga Nyamanche, Tini Nyamanche na Mang'era Nyamanche na wengine ni Machera Waryoba, Sasi Kibuche na Amos Mwita. Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Jaji wa Mahakama Kuu, Ephery Kisanya, katika kikao cha Mahakama Kuu ya Musoma kilichoketi Tarime kusikiliza kesi tatu tofauti za mauaji.

Awali, Wakili wa Serikali Frank Nchanila, alidai kuwa mwanafamilia mmoja, Thobias Chacha, aliachiwa huru baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha alivyohusika katika maauji hayo Julai 22, 2018 usiku katika Kijiji cha Kenokwe Mugumu, Serengeti.

Watuhumiwa hao wanadaiwa walivamia mji wa Zabron Mokono, aliyekuwa Mwenyekiti wa Ritongo, kumkata mapanga na kusababisha kifo chake kutokana na chuki.

Mwingine aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa ni Kegokora Jackson, aliyemuua Nyaimwa Mhochi kwa kufuata panga nyumbani kwake na mishale na kumvamia kwa kumkata mapanga wakiwa wanakunywa pombe kilabuni, Juni 1, 2018 katika kijiji cha Nyaisense Mugumu, Serengeti.

Ilidaiwa, washtakiwa walimuua Mwita Machera Waryoba, Novemba 4, 2015 kwa kumchinja na kumtenganisha kichwa na kiwiliwili huku mwili wake wakiutupa vichakani.

Wakili Nchanila alidai kuwa watuhumiwa wote watatu akiwamo baba wa marehemu, Machera Waryoba, ilidaiwa alimpa kijana wake ambaye kwa sasa ni marehemu Mwita, ng'ombe kwa ajili ya mahari ya kuoa mke na badala yake aliwauza na pesa kulewa pombe na kushinda kuoa mke, kitendo kilichomchukiza baba yake huyo ambaye alipanga mauaji ya kijana wake huyo.

Ilidaiwa mahakamani kuwa aliwaita kwenda shambani kukata miti ya kuchoma mkaa na kuwaamuru Sasi na Amos Mwita, kumkamata kijana wake miguu na mikono na kisha kumkata kichwa na baadaye kuwaonya wasitoe siri.

Mwili wa marehemu ulipatikana ukiwa umetenganishwa na kichwa huku fuvu likiwa limeliwa na wanyama baada ya siku tatu katika msako uliofanywa na wanakijiji. Ilidaiwa pia kuwa washtakiwa walilazimishwa kuonyesha eneo kulikofanyika mauaji hayo na kukuta kiwiliwili hicho cha Mwita.

Upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi sita huku upande wa utetezi ukileta mashahidi wanne na kutetewa na mawakili wa kijitegemea Tumaini Kigombe na Rebeka Magige.

Washtakiwa katika kesi hiyo Khanga Nyamanche, Tin Nyamanche na Mangera Nyamanche, walipeleka mashahidi saba huku upande wa utetezi ukileta mashahidi sita.

Jaji Ephery Kisanya, alisema kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka bila kuacha shaka lolote, washtakiwa sita kati ya saba walifanya mauaji ya kukusudia na adhabu yao ni kunyongwa hadi kufa, huku mtuhumiwa Thobias Chacha akiachiliwa huru baada ya ushahidi kushindwa kuthibitisha kuhusika kwa kuwa ushahidi ulidai ulisikia sauti bila ya kumuona.

# TAKUKURU yataka kibano taasisi za 'mikopo umiza'

**Na Rose Jacob, MWANZA**

SERIKALI imeshauriwa kuchukua hatua za kisheria dhidi ya taasisi na watu binafsi wanaojihusisha na huduma ya utoaji mikopo ambao hawana leseni ya kufanya biashara hiyo.

Wakopeshaji hao wamedaiwa kuwa matapeli kwa kuuza dhamana za wateja wao walioshindwa kurejesha mikopo bila kuzingatia thamani ya mali husika, kukiuka taratibu za minada kwa kutangaza mnada jioni na kuuza asubuhi, jambo ambalo linamnyima haki mkopaji na kujikuta amepoteza mali ya Sh. milioni 50 kwa deni la Sh. milioni tano.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Stenga, baada ya kufanyika uchunguzi kuanzia Julai 2015 hadi Juni 2020 na kubaini ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Alisema hayo katika maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu jijini Mwanza, na kuongeza kuwa wananchi wengi wana matatizo hivyo wakopeshaji wanatumia fursa hiyo kuwaibia.

"Wananchi pamoja na watumishi, wamekuwa wakinyanyaswa sana na watoa mikopo wasio rasmi kwa kuuza mali za wadhamini, kuacha mali za wakopaji na taasisi hizo za fedha zimekuwa zikifanya utapeli kwa kutumia njia ya kukataa kutoa hesabu za salio la deni la mkopo kwa wateja wao," alisema Stenga.

Alisema serikali na waajiri walinde maslahi ya wananchi na watumishi, dhidi ya taasisi za fedha zinazowadhulumu kwa njia ya kutoa mikopo kwa kuwapatia elimu inayowataka wakopaji kutokudhamini mikopo kutoka kwenye taasisi zisizotambulika..

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema kwa mujibu wa sheria zinazosimamia taasisi za fedha, mtu binafsi na taasisi yoyote haziruhusiwi kutoa huduma ya mikopo yenye riba bila leseni, wakifanya hivyo bila kutambulika kisheria basi mkopaji akishindwa kumlipa hatakuwa na uhalali wa kumdai.

"Watu wamekuwa wakiishi kiujanja ujanja, hawataki kufuata taratibu za kisheria...wewe kama unaweza kutoa huduma ya mikopo basi fuata maelekezo na miongozo husika ili ufanye biashara yako kwa amani, Rais John Magufuli kila siku anasisitiza tuwe waadilifu, lakini watu hawasikii wala hawana hofu ya Mungu," alisema Mongella.

# Mwanafunzi wa kike aibuka kidedea Ardhi

**Na Elizabeth Zaya**

MWANAFUNZI wa kike, Jasmine Mndeme, ameibuka mwanafunzi bora zaidi kati ya wahitimu 926 wa Chuo Kikuu cha Ardhi mwaka huu.

Jasmine alihitimu Shahada ya kwanza ya Usanifu, Gharama na Usimamizi wa Majengo.

Akizungumza baada ya mahafali ya 14 ya Chuo hicho, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Evaristo Liwa, alisema siri ya wanawake kufanya vizuri katika chuo hicho imetokana na nidhamu ya masomo waliyonayo.

Alisema wanafunzi wa kike wanaojiunga na chuo hicho wamekuwa na nidhamu kuliko wa kiume hususani katika kuzingatia yale wanayoelekezwa katika masomo yao na kuepuka kuzurura ovyo.

Prof. Liwa alisema kati ya wanafunzi hao waliohitimu mwaka huu, asilimia 43 walikuwa wanawake na wote wamefanya vizuri katika masomo yao na kutunukiwa tuzo.

"Nina furaha sana kwa sababu asilimia yote ya wanawake katika Chuo cha Ardhi, wamefaulu vizuri, na mara nyingi wanaoshindwa ni wanaume, lakini wanawake wote wamekuwa wakifanya vizuri, na hili nimelithibitisha,"alisema Prof. Liwa.

"Kati ya wanafunzi 87 waliofanya vizuri zaidi katika masomo yao na kutunukiwa zawadi, wanaume walikuwa ni 44 na wanawake ni 43, na asilimia 100 ya wanawake wanaojiunga na chuo chetu wanafanikiwa kuhitimu, na hii ya mwanamke kuwa wa kwanza mwaka huu imetupa faraja kubwa sana," alisema.

Alisema kwa miaka miwili mfululizo, idadi ya wanawake katika chuo hicho imekuwa ikiongezeka tofauti na ilivyokuwa katika miaka mingine ya nyuma.

Prof. Liwa alisema ni vema imani iliyokuwa imejengeka zamani ya kwamba masomo yanayofundishwa katika chuo hicho ni ya wanaume ikabadilishwa kwa kuwa kwa sasa kuna idadi ya wanawake imeongezeka na wanafanya vizuri zaidi.

"Nawaomba wanawake waje Chuo cha Ardhi na wasiogope na idadi ya wanawake wanaoomba inapanda, na kuna masomo ambayo wanawake ni wengi kuliko wanaume." Aliwataka wahitimu hao kuhakikisha wanatumia taaluma yao vizuri katika kuleta matokeo chanya ya katika uchumi wa nchi.




The Guardian Nipashe
MWANGA WA JAMII

TWO UNBEATABLE DEALS IN ONE PLACE



Free Delivery at your Door Step + more than 20% off on 1 year upfront Subcription

| Number of Dailies | Cover Price (Tsh) | Offer Price(Tsh) | Your Saving (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 1 Months | 26,000/= | 24,000/= | 2,000/= |
| 3 Months | 79,000/= | 70,000/= | 9,000/= |
| 6 Moths | 157,000/= | 130,000/= | 27,000/= |
| 1 Year | 314,000/= | 250,000/= | 64,000/= |

Please mention the start date from when you want to receive your subscription

**For enquiry**,Please contact Subcription Supervisor - **Sophia Lema**

+255713852323

**Email:** subscription@guardian.co.tz

Offer valid from 1st Dec 2020 to 31st Dec 2020

Terms & Condition Apply



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu ziheshimu, zitangulize maslahi wachezaji dirisha hili

**RASMI** usajili wa dirisha dogo kwa klabu za Tanzania Bara kwa ajili ya kuongeza nguvu, kuimarisha vikosi ama kuziba upungufu uliojitokeza kwenye mzunguko wa kwanza kwa timu za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza, linafunguliwa kesho Jumanne Desemba 15.

Tayari baadhi ya klabu zikiwamo Simba na Yanga, zilishaingia mikataba na baadhi ya wachezaji hivyo zinachosubiri ni dirisha hilo kufunguliwa hapo kesho ili kukamilisha taratibu zote za Shirikisho la Soka nchini (TFF) na kuanza kuwatumia.

Yanga ilikuwa ya kwanza kumpa mkataba kiungo mshambuliaji raia wa Burundi, Saido Ntibazonkiza, kabla ya Simba kuingia mkataba na kiungo mkabaji, Mganda Thadeo Lwanga, huku pia klabu hizo zikiendelea kuhusushishwa na baadhi ya wachezaji.

Pamoja na mchakato huo kuanza kwa baadhi ya klabu, tunatambua katika dirisha hili kama yalivyo mengine, wapo wachezaji wataachwa kutokana na mikataba yao kumalizika ama watatemwa kwa sababu ya viwango vyao kushuka au kutolewa kwa mkopo, ili kutoa nafasi kwa nyota wapya ambao klabu husika zinaamini wanaweza kuzisaidia kutimiza malengo yao ya msimu huu endapo zitawasajili. Hata hivyo, ikumbukwe pia kutemwa kwao hakuwezi kuwa safari ya mwisho kisoka kwani upo msemo wa wahenga usemao "ukisema wa nini, mwenzako anajiuliza atampata lini" na unaweza kuonekana hufai hapa ila kwingineko ukawa lulu.

Kwa maana hiyo, wachezaji watakaotemwa hawana budi kutambua hayo ndiyo maisha ya soka na kinachotakiwa ni kuendeleza juhudi zao katika kupambana zaidi kwa klabu mpya zitakaowasajili ili kuthibitisha ubora wao.

Aidha, tunafahamu wazi zipo klabu ambazo zimetega mitego yao zikisubiri wachezaji watakaotemwa hususan kutoka kwa klabu kubwa ili ziwasajili jambo ambalo Nipashe tungependa kuona klabu zote zikitangulia kwanza kutangaza wachezaji zinaowatema kabla ya kuanza kusajili wapya ili kuwapa fursa ya kujiweka sokoni mapema. Hatutarajii kuona wachezaji wakutemwa katika dirisha hili wakiwa wa mwisho kutangazwa baada ya klabu husika kufanya usajili kwa kuwa kufanya hivyo ni kutowatendea haki hasa ikizingatiwa soka ni maisha yao.

Lakini pia tunapenda kuwakumbusha wachezaji wasiopata nafasi katika timu zao, kuomba kutolewa kwa mkopo kwingineko ili kulinda vipaji vyao badala ya kuendelea kubweteka tu na maslahi hapo walipo, na kati hilo pia klabu zinawajibu wakuridhia maombi hayo kwa maslahi ya wachezaji husika.


Tunatoa rai hiyo mapema kwa kutambua kuwa wapo baadhi ya wachezaji ambao walishawishika kusajiliwa na baadhi ya klabu kutokana tu na kuahidiwa dau kubwa ama kufuata mapenzi yao kwa klabu husika, lakini baadaye wamejikuta wakisugua benchi katika kila mechi ama kuishia kupata nafasi chache dimbani wakitokea benchi. Hivyo, wachezaji kama hawa, hawana budi kuomba kuondoka ama kutolewa kwa mkopo badala ya kuendelea kusugua benchi au kusubiri kucheza wakitokea benchi katika kila mechi jambo ambalo linachangia kushusha kwa viwango vyao.

Aidha, kwa klabu za Simba na Namungo FC mbali na michuano ya ndani; Ligi Kuu Bara na Kombe la Shirikisho la Soka nchini (FA Cup) linalotarajiwa kuanza hivi karibuni, zinapaswa kuwa makini zaidi katika dirisha hili dogo la usajili kutokana na jukumu kubwa lililo mbele yao la kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba tayari imeitoa Plateau United ya Nigeria katika raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Namungo FC ikiitupa nje Al-Rabita ya Sudan Kusini nakutinga raundi ya kwanza ambapo zitakuna na FC Platinum ya Zimbabwe na El Hilal Obeid ya Sudan, hivyo usajili wao unapaswa kuwa makini zaidi.

Lakini pia, matarajio yetu ni kuona usajili wa dirisha hili, kanuni na sheria zikifuatwa huku klabu zikitanguliza mbele maslahi ya wachezaji kwa kuwasikiliza maoni yao hususan wale wasiopata nafasi katika kikosi cha kwanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu zisisajili kwa kukomoana dirisha dogo

Na Adam Fungamwango

**NIMEANZA** kusikia makocha wengi wakisema kuwa watasajili baadhi ya wachezaji kipindi cha dirisha dogo ambalo huenda likafunguliwa Jumanne ya Desemba 15 na Shirikisho la Soka nchini (TFF).

Nimemsikia Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, akisema ni lazima asajili wachezaji kipindi hicho ili kuinusuru timu yake ambayo ni kama imekuwa jamvi la wageni, kila timu yenye uwezo wake inajipigia tu goli nyingi.

Hata Kocha Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze pia, ameonyesha ni kama anahitaji mchezaji au wachezaji hivi kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chake.

Nadhani si hao tu, inavyoonekana kipindi cha dirisha dogo msimu huu kutakuwa na hekaheka kwa baadhi ya timu kusaka wachezaji kwa ajili ya kuongezea nguvu vikosi vyao, sehemu ambazo zitakuwa na upungufu.

Ligi Kuu ya msimu huu imeonekana kuwa ni ngumu na baadhi ya timu zimeonekana kutetereka, hivyo sasa kimefika kipindi cha kurekebisha upungufu huo.

Timu kama Ihefu, inayoshika mkia, wala haitakiwi kupepesa macho, viongozi wa klabu hiyo wanatakiwa kuingia mifukoni mwao na kusajili wachezaji wazoefu kwenye Ligi Kuu ili wakiimarishe kikosi chao.

Nawaibia siri tu kuwa wachezaji kama Kelvin Yondani, bado yupo sokoni na hata Mrisho Ngassa kama wanamhitaji wanaweza kumtoa alipo Ndanda na kumrejesha kwenye Ligi Kuu.

Hao ni mfano tu wa wachezaji wengi ambao kwa sasa wapo ubaoni, na hawakupata kusajiliwa na timu yoyote kwa sababu mbalimbali kama kuchelewa, majeraha na mengine yanayofanana na hayo.

> **Hao ni mfano tu wa wachezaji wengi ambao kwa sasa wapo ubaoni, na hawakupata kusajiliwa na timu yoyote kwa sababu mbalimbali kama kuchelewa, majeraha na mengine yanayofanana na hayo.**

Timu zingine ambazo naziona kabisa zinatakiwa ziende sokoni ni Mwadui FC, JKT Tanzania, Coastal Union, Azam FC, na hata Dodoma Jiji.

Kuna zinazotakiwa zifanye usajili wa wachezaji mpaka watano, lakini zingine zinatakiwa zifanye usajili wa mchezaji mmoja au wawili tu.

Hapa ninavyoandika, tayari klabu za Simba na Yanga zimewapa mikataba wachezaji na wanachosubiri ni kufunguliwa kwa dirisha tu. Yanga ilikuwa ya kwanza kumpa mkataba Saido Ntibazonkiza raia wa Burundi, wakati Simba imeingia mkataba na Thadeo Lwanga raia wa Uganda.

Kwa upande wa Simba, wanasajili baadhi ya wachezaji kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa, Yanga nayo ikitaka kuleta majembe kwa ajili ya kuongeza nguvu mbele, huku Azam nayo ikiwa na pengo la Prince Dube ambaye ameumia.

Kila timu sasa isajili kwa kuangalia upungufu wake na si kuzoazoa wachezaji ambao baadaye wanakuwa hawana faida wala tija kwenye timu na kuwa mizigo.

Kwanza kabisa kama kocha anaona timu iko vizuri, basi lazima kuingia sokoni kipindi hiki kwa sababu usajili si fasheni kwamba kila nguo mpya ikitoka basi lazima ununue.

Lakini hiki si kipindi cha kuacha robo au nusu ya wachezaji na kusajili wengine wapya kama Yanga ilivyofanya msimu uliopita.

Ikumbukwe kuwa huu ni usajili tu wa kuziba upungufu na si kusajili lundo la wachezaji ili wanachama na mashabiki wawasifie viongozi kuwa ni watu hatari kwa usajili, au kusajili kwa sababu kuna timu inamtaka.

Imefika wakati viongozi wa klabu wabadilike, wasajili kutokana na mahitaji tu na si kwa sababu za siasa za mpira.

Lakini pai umefika wakati sasa wawe wanazionea huruma klabu, waangalie gharama kubwa zinazoingiwa bila sababu yoyote. Wawaonee huruma na watu wanaojitolea kutoa pesa kwa ajili ya usajili pia.



Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Saidi Makiniligo, akitoa maelekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, ya makundi ya vyakula vyenye lishe na namna ya kuandaa vyakula hivyo wakati wa ufunguzi wa kitengo cha kutolea huduma za lishe katika Hospitali ya Rufani Shinyanga. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Madiwani waonywa kufukuza watumishi

**Na Happy Severine, SIMIYU**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amewataka madiwani wa halmashauri zote katika mkoa huo, kutokuwa chanzo cha migogoro kwenye maeneo yao, huku akipiga marufuku tabia ya kuazimia kuwafukuza watumishi bila ya sababu za msingi.

Amesema kuwa hatokuwa tayari kukubali madiwani wa halmashuari yeyote kukaa kikao na kuanza kuazimia kumfukuza mtumishi yeyote wa serikali awe mkurugenzi, mkuu wa idara au kitengo na badala yake watumie njia sahihi katika kufanya uamuzi huo.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao kazi kilichofanyika mjini Bariadi ambacho kiliwashirikisha madiwani wote wa mkoa mzima, viongozi wa wilaya na halmashuari, wakiwamo watumishi wa serikali, viongozi wa dini, vyama vya siasa kwa lengo la kuelezea mwelekeo wa mkoa kwa miaka mitano ijayo.

Aliwaeleza madiwani hao kuwa na upendo kwa watumishi wao na kushirikiana nao kila wakati, na siyo kutumia nafasi yao kutaka kuwafukuza au kuwakataa wasifanye kazi kwenye halmashuari zao.

Alisema kama wataona kuna mtumishi yeyote wa serikali utendaji kazi wake siyo mzuri, washauriane kwanza na ofisi yake kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa ili kuona njia gani sahihi ya kumwajibisha mtumishi huyo.

" Mkitaka kufanya kazi vizuri wapeni heshima watumishi wa serikali, lakini kama mnakwenda kwenye baraza kuazimia mtu, hamtamtoa, hilo niwaambie niko hapa mwenyewe, hakuna mtu utaazimia umtoe, hautaazimia mkurugenzi, mkuu wa idara wala ofisa," alisema Mtaka.

" Fanyeni kazi kama kuna jambo kwenye halmashuari uongozi wa mkoa upo, katibu tawala yupo, mkuu wa mkoa yupo... tuambieni, tukishindwa tunapeleka TAMISEMI , vitumieni vyombo vya dola, TAKUKURU na wengine na siyo kuazimia," alisisitiza Mtaka.

Aliwataka madiwani hao kwenda kuwatumikia wananchi na kutatua kero zao, kama ambavyo waliwaahidi wakati wa kampeini na siyo kuanzisha migogoro isiyokuwa na tija huku akiwasisitiza kutambua kuwa kipaumbele cha mkoa ni elimu kwanza.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Simuyu, Miriam Mmbaga, aliwataka viongozi hao wapya wa kisiasa kutumia muda mwingi kuwatumikia wananchi kwa kuzingatia sheria ya maadili kwa viongozi wa umma.

Naye Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Simuyu, Joshua Msuya, aliwataka viongozi hao kutojihusisha na vitendo vya rushwa, badala yake wawe wasimamizi wa fedha za serikali ambazo zinapelekwa kwenye vijiji na kata zao.

# Waadau wa habari wapewa changamoto ya wakimbizi

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa habari hususan waandishi wa habari wametakiwa kuandika habari kuhusu wakimbizi, ili kuongeza kumbukumbu za maandishi na kusaidia kwenye utafiti.

Mhadhiri wa Shule Kuu ya Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Khoti Kamanga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam kwenye semina ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuripoti habari hizo.

Prof. Kamanga ambaye pia ni mshiriki wa kituo cha masuala ya wakimbizi, Centre for the Study of Forced Migration katika shule hiyo, alisema taarifa zilizoandaliwa kuhusu wakimbizi waliopo barani Afrika, zinaandaliwa na mataifa ya nje.

"Taarifa kuhusu wakimbizi ambao kwa idadi kubwa Tanzania huwapokea zaidi tangu miaka ya 1950 hazijaandaliwa, hii inatokana na uwekezaji mdogo, uchumi mdogo na uhaba wa wahadhiri wa kufanya hivyo. Kunahitajika angalau Dola 500 kufanya utafiti, kufika maeneo ya wakimbizi na muda wa kuandaa na kuweka kwenye maandishi, vitabu, hivi sasa tunategemea utafiti uliofanywa na nchi za nje, utafiti ambao hatuna miliki nao," alisema Prof. Kamanga.

Alisema kumbukumbu zozote hupatikana katika machapisho na si lazima ziwe katika vitabu, huwapo kwenye magazeti, kupitia makala na habari na kusaidia kufanyia utafiti.

"Mfumuko wa wakimbizi ulianza miaka ya 1940, ila hakuna kumbukumbu, wazee wetu wana kumbukumbu hizi kichwani wanatembea nazo," alisema Prof. Kamanga. "Magazeti pia ni kumbukumbuku nzuri na rahisi, itasaidia kutumia kama nchi na kujivunia tulichokiandika wenyewe cha kwetu." Janemary Ruhundwa ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Dignity Kwanza wa shirika lisilo la kiserikali linaloshughulika na masuala ya wakimbizi nchini, alisema kwa kipindi cha miaka 60, Tanzania imefanya mambo makubwa katika kuwapokea wakimbizi hivyo kunahitajika machapisho kutunza kumbukumbu.

"Kumbukumbu kuhusu wakimbizi walianza kupokelewa tangu miaka 60 iliyopita hazijaandikwa, tunahitaji kuanika ili kusaidia katika utafiti na kizazi kijacho," alisema Ruhundwa. Alisema shirika hilo linatarajia kuandaa machapisho ikiwamo kitabu, kuelezea masuala mbalimbali ya wakimbizi na tayari limeanza kufanya utafiti, kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu muundo wa uandishi.

# Shule kongwe yakarabatiwa kwa mil. 798/-

**Na Gideon Mwakanoya,**
TUNDURU

SERIKALI imetoa Sh. milioni 798 kwa ajili ya kukarabati shule kongwe ya sekondari ya wavulana Tunduru mkoani Ruvuma yenye wanafunzi zaidi ya 700, ambayo ilianzishwa mwaka 1978.

Mkuu wa shule hiyo, Limia Ausi, amesema Serikali imetoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kukarabati madarasa, mabweni, ujenzi wa choo kipya, banda la mlinzi na kwamba nyumba za walimu hazihusiki katika ukarabati huo.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo, ukarabati umeanza Agosti mwaka huu, na kwamba unafanyika huku ratiba ya masomo kwa wanafunzi ikiendelea, hivyo kusababisha kazi hiyo kwenda polepole, lakini bila kuathiri masomo.

"Inatulazimu wanafunzi kuwahamisha katika baadhi ya madarasa na wakati madarasa yao yanaendelea kukarabatiwa," alisema na kuongeza kuwa ujenzi umefikia zaidi ya asilimia 90.

Amesema ukarabati upo katika hatua za mwisho, na kwamba baadhi ya mambo yaliyokwishakamilika ni jengo la utawala, vyumba vya madarasa 16 na mabweni sita.

Alieleza kuwa shule hiyo ilijengwa na Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 1978 kwa ajili ya watoto wa wakimbizi waliokuwa walihifadhiwa nchini wakati wa harakati za ukombozi katika nchi za kusini mwa Afrika.

Hata hivyo amesema baada ya harakati za ukombozi kukamilika UN waliikabidhi shule hiyo serikalini, ambapo serikali ilianza kuwachukua wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali nchini na kuwapeleka Tunduru kwa ajili ya elimu ya kidato cha kwanza hadi cha nne.

Mkuu huyo wa shule kwa niaba ya walimu aliishukuru serikali kwa kutoa fedha za ukarabati kutokana na awali kuwa na majengo chakavu, ambayo yalikuwa kero kwa wanafunzi na walimu.

Abdalanus Sala mwanafunzi wa kidato cha sita, ameishukuru serikali kwa kumaliza kero ya mazingira magumu ya miundombinu ya madarasa, vyoo na mabweni, na kwamba wanafunzi hivi sasa wanasomea kwenye mazingira bora.

## ARU yabuni teknolojia mkaa mbadala

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu Ardhi (ARU), kimebuni teknolojia ya utengenezaji mkaa mbadala unaotokana na taka ngumu zikiwamo mabaki ya mazao ili kuongeza ujuzi na ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu na wakulima wadogo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Evaristo Liwa, wakati akizungumza kwenye mahafali ya 14 ya chuo hicho na wanafunzi 927 walitunukiwa shahada za awali, shahada za uzamili, shahada za uzamivu nne.

Alisema mradi huo umesaidia kupanga, kupima na kutoa hatimiliki katika mji wa Mbarali na kupatikana kwa maeneo ya viwanda vidogo vidogo kwaajili ya utengenzaji wa mkaa na miundombinu ya kusafirisha malighafi za viwanda hivyo.

Alitaja fursa zingine zilizopatikana kuwa ni hatimiliki na mitaji, kupunguza migogoro ya ardhi, kudhibiti magonjwa ya mlipuko na athari zitokanazo na tabia nchi.

Profesa Liwa alisema chuo pia kimefanya utafiti wa kuboresha matumizi na mbinu mpya za umwagiliaji katika bonde la mto Rufiji ili kuleta tija na kuongeza uzalishaji katika Wilaya ya Iringa pamoja na kutatua changamoto mbalimbali za matumizi ya maji katika Mto Rufiji.

Profesa Liwa alisema chini ya ufadhili wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), chuo kimefanya utafiti kuhusu teknolojia ya asili ya ujenzi wa nyumba zinazostahimili matetemeko ya ardhi katika mji wa Dodoma na utafiti huo utawezesha kutumia taaluma hiyo kwenye ubunifu wa majengo ya kisasa ya mkoa huo.

Alisema mafanikio ya chuo hicho yasingewezekana kama siyo juhudi za pamoja baina ya chuo na wadau katika maendeleo ya sekta ya elimu wa ndani nje ya nchi. Alitaja wadau hao kuwa ni serikali, SIDA ya Sweden, GIZ na DAAD ya Ujerumani, Norway, Denmark na China huku akitambua mchango mkubwa wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuendeleza na kutatua changamoto za Chuo Kikuu Ardhi (ARU), jambo ambalo limewezesha utoaji wa elimu bora na ukuaji wa taaluma.

"Kipekee niwapongeze wahitimu wote kwa hatua hii muhimu katika historia na maendeleo yenu binafsi na taifa kwa ujumla kwa kuwa natambua safari ya kufikia mafanikio haya haikuwa rahisi, lakini juhudi kubwa na nidhamu ndiyo msingi wa mafanikio haya," alisema.

Alisema kwa mwaka wa masomo wa 2020/21, ARU imedahili wanafunzi 1,653 wa mwaka wa kwanza kwa shahada za awali na wanafunzi 97 kwa shahada za uzamili ikiwa ni ongezeko la asilimia nane ikilinganishwa na mwaka 2019/2020.

Alisema chuo kimeanzisha programu mpya 13 za shahada za awali, uzamili na uzamivu wakizingatia uhitaji wa soko la ajira na Tanzania ya uchumi wa viwanda.



Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uhusiano Tawi la Oysterbay, Witness Kileo, kuhusu uwezeshaji unaofanywa kwa Wanawake kupitia CRDB Malkia, wakati wa Mkutano Mkuu wa Pili na Madirisha uliofanyika jumamosi hii katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam. Wanawake zaidi ya 1,000 wamehudhuria mkutano huo na kupata elimu juu ya fursa mbalimbali zinazotolewa na Benki hiyo ikiwamo; Mikopo ya Wanawake Wajasiriamali (WAFI), Akaunti ya Malkia na Huduma ya Malkia Rafiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu TRA kuvuka lengo mapato Simiyu

**Na Happy Severin,** BARIADI

MAMLAKA ya Mapato (TRA), Mkoa Simiyu, imeleza sababu za kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato idara ya kodi za ndani kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kuwa ni kuongezeka kwa ulipaji kodi kwa hiari kupitia uwasilishaji wa ritani sahihi za kodi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha kuanzia Julai 2019 hadi Juni 2020, mkoa ulipangiwa kukusanya jumla ya Sh. bilioni 8.7 na kufanikiwa kukusanya jumla ya Sh. bilioni 8.6 ikiwa ni sawa na asilimia 99.5 ya lengo.

Aidha, katika idara ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2018/2019 lengo lilikuwa kukusanya Sh. bilioni 3.5, makusanyo yalikuwa Sh. bilioni 5.9 sawa na asilimia 169, 2019/2020 lengo lilikuwa Sh. bilioni 8.7, makusanyo yalikuwa Sh. bilioni 8.6 sawa na asilimia 99.5.

Akieleza sababu hizo, Meneja wa TRA Mkoa wa Simuyu, Michael Nsobi, alisema ongeko hilo limechangiwa na malipo ya kodi husika kwa wakati hasa kutoka katika sekta ya maliasili na utalii, sekta ya viwanda pamoja na sekta ya chakula na malazi.

"Mbali na sekta hizo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa mapato pia mpango wa serikali wa ukusanyaji wa madeni bila riba," alisema Nsobi na kuongeza:

"Kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha 2020/2021 Mkoa wa Simiyu umepangiwa kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 9.6 kwa idara ya kodi za ndani kwa mchanganuo wa kodi za kawaida, kodi za majengo pamoja na ushuru wa mabango."

Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Novemba mwaka 2020 mkoa ulipangiwa kukusanya lengo la jumla ya Sh. bilioni 3.6 na kufanikiwa kukusanya Sh. bilioni 3.4 ikiwa ni sawa na asilimia 93.4 ya lengo.

Baadhi ya wafanyabiashara katika soko kuu la Mji wa Bariadi walisema licha ya ongezeko hilo la mapato, bado kuna mapato mengi yanapotea kutokana na wauzaji kushindwa kutoa risiti na wanunuzi kutokudai risiti.

"Ni haki yetu kulipa kodi japo kuna muda unaona kuwa ni hasara, lakini tukizingatia utoaji wa risiti, tutaziba mianya mingi ya upotevu wa mapato," alisema John Mapanduzi, mfanyabiashara wa vifaa vya ujenzi.

# PASS Trust yahamasisha wanawake kilimobiashara

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA binafsi ya kusaidia kilimo (PASS Trust), imewataka wajasiriamali wanawake wa kilimo kutumia fursa za bidhaa za PASS kujiiunua kiuchumi kwa kujiingiza kwenye kilimobiashara.

Akizungumza katika mkutano wa mwaka wa Madirisha Women Cooperative Society, 2020 uliofanyika jijini Dar es Salaam na kufunguliwa na Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Peter Pinda, Mkurugenzi Mtendaji wa PASS, Nicomed Bohay, alisema wanawake wana mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi kupitia shughuli za kilimo.

Bohay alisema PASS Trust ambayo inasaidia wanawake kwenye kilimobiashara, itaendelea kuhakikisha wanafaidika na mikopo iliyowekewa dhamana mpaka asilimia 80 tofauti na mingine ambayo hutoa dhamana ya asilimia 60.

"Tunafahamu jinsi wanawake wanavyohangaika, wanavyofanyakazi kwenye sekta ya kilimo. Mikopo yetu yenye dhamana ya asilimia 80 itawasaidia kupata fedha za kusaidia uzalishaji," alisema Bohay.

Madirisha Women Cooperative Society ni umoja wa wanawake wanaojishughulisha na kilimobiashara ambao wanazalisha bidhaa mbalimbali kibiashara. Chama hicho kinawezesha wanawake kama kikundi kupata masoko na kwa bei nafuu.

"Hii inasaidia PASS Trust kuwezesha vikundi hivi kupata dhamana ya mikopo. Kupitia PASS, hawa wanawake wanaweza kupata fedha na kukuza bidhaa zao na kuziuza kwa wingi na faida watakayopata itasaidia familia zao kuboresha maisha yao," alisema Bohay.

Zaidi ya wanawake 1,200 waliohudhuria mkutano huo walifurahia jinsi dhamana inayotolewa na PASS Trust kuwapendelea kwenye kilimobiashara.

PASS Trust inashirikiana na zaidi ya benki 14 za kibiashara nchini na zimesaidia wanawake na wajasiriamali wanaojihusisha na kilimobiashara ambao walikuwa hawakopesheki.

Mkazi wa Kahama, maarufu kwa jina la Mama Mageuzi ni kati ya wanawake walionufaika na mfumo wa dhamana ya PASS, ambaye kwa sasa anatambulika kama milionea kwenye kilimobiashara, baada ya kuanza kidogo na sasa anamiliki mashine ya mpunga na kiwanda cha ufungashaji kwa kusaidiwa na PASS Trust.

Wengine ni Mama Agnes Adam Mwakatole kutoka Njombe, mkulima wa mahindi na Chetu Omari Korongo, mkulima wa mpunga.

Zaidi ya wakulimabiashara milioni 1.5 wamefaidika na PASS Trust tangu mwaka 2002 ilipoanza kutoa huduma. Asilimia 45 ya wanufaika ni wajasiriamali wanawake wanaojihusisha na kilimo cha mnyororo wa thamani.

Mwaka 2019 wajasirimali 267,000 wa kilimobiashara walifaidika na dhamana ya PASS Trust, asilimia 42 ya wanufaika walikuwa wanawake.

Katika kipindi cha 2018-2022 mipango mikakati ya PASS Trust ni kunufaisha wanawake zaidi kwenye kilimobiashara.

# Jeshi, DUWASA washirikiana kulinda bonde la Makutupora

**Na Frank Monyo**

WAKAZI wa maeneo jirani na bonde la Makutupora jijini Dodoma, wametakiwa kuacha mara moja shughuli za kilimo na ufugaji ili kulitunza bonde hilo ambalo ni chanzo pekee cha maji kinachotegemewa na makao makuu ya nchi.

Mkuu wa kituo cha uzalishaji maji Mzakwe, Peter Shemwelekwa, alisema katika jitihada za kulinda rasilimali hiyo, Mamlaka ya Maji Dodoma (DUWASA) kwa kushirikiana na Ofisi za Bonde la Wami Ruvu ambalo linasimamia bonde la Makutupora mara kwa mara wamekuwa wakichukua hatua kuhakikisha chanzo hicho kinatunzwa kwa ajili upatikanaji wa maji wa uhakika.

"Makutupora ni chanzo pekee cha maji kinachotegemewa na jiji letu, kuna shughuli ambazo zinatakiwa zisifanywe katika bonde hili, kama ukataji wa miti kwa ajili ya kuchoma mikaa, kilimo cha kutumia mbolea na ulishaji mifungo. Tunahitaji kulitunza hili bonde hili tuwe na uhakika wa kuwapatia maji wananchi wa Dodoma kwa wakati wote,"alisema.

Akizungumzia hali ya utunzaji wa rasilimali za maji jijini humo mwishoni mwa wiki, aliwaambia waandishi kutoka vyombo mbalimbali vya habari waliotembelea bonde na Wami Ruvu kuripoti juu ya utunzaji wa maji.

Alisema kazi hizo zinafanywa kupitia Mradi wa Kuendeleza Utumiaji wa Pamoja wa Rasilimali Maji (WARIDI) unaofadhiliwa na Shirika la Marekani la Misaada ya Kimataifa la USAID.

Shemwelekwa alisema kutokana na Dodoma kuwa makao makuu ya nchi kumekuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya maji na kwamba uwezo wa uzalishaji maji katika bonde hilo ni lita milioni 61.5 kwa siku kutoka katika visima 18 vilivyopo ndani ya jiji hilo.

"Hapa tulipo, tupo katika moja wapo ya kisima kirefu namba 118/75 ambacho kilichimbwa mwaka 1975, kina uwezo wa kuzalisha maji lita 175,000 kwa saa ambayo yanapelekwa kwenye matangi kwa ajili ya kusambazwa kwa wananchi wa Dodoma," alisema Shemwelekwa.

Aliongeza kuwa chanzo cha maji bonde la Makutupora kwa sasa ndicho chanzo pekee kinachotegemewa katika jiji la Dodoma kutokana na mahitaji ya maji kuongezeka kwa kasi kutoka na ongezeko la watu.

Alisema kuwa zipo sheria ambazo zimewekwa kwa yeyote atakayekamatwa akifanya shughuli hizo ndani ya eneo la bonde ambalo DUWASA kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kambi ya Makutupora wanashirikiana kwa karibu kulinda chanzo hicho.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Vallery Chamlungu, akipokea Tuzo ya mshindi wa kwanza kwa Mamlaka za Udhibiti katika uwasilishaji mzuri wa taarifa za mwaka za mahesabu kwa mwaka 2019. Tuzo hizo zimetolewa tarehe 5 Desemba 2020 na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA). Kulia ni Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka ya Usafiri wa Anga Teophory Mbilinyi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu wa vyuo vikuu wapewa ujuzi zaidi kujiajiri

**Na Christina Mwakangale**

WAHITIMU wa vyuo vikuu pamoja na kufunzwa katika fani mbalimbali kitaaluma, wanaelezwa kuwa wanakosa ujuzi wa ziada, upungufu unaowakwamisha na kushindwa kupambana katika soko la ajira.

Haya yanaelezwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS) Francis Kiwanga, na kusema kuwa ili kukabiliana na upungufu huo, wanatoa mafunzo kwa vijana wa vyuo vikuu ikiwamo kuwakutanisha wabobezi kwenye biashara ili kuondoa ombwe katika soko la ajira.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki ambayo yamepewa jina la 'Giving Tuesday', alisema lengo ni kuwaongezea uzoefu kukabiliana na tatizo la ajira, hasa kwa wahitimu wa vyuo vikuu.

'Giving Tuesday ni siku ya kutoa shukrani kwa jamii hususan kwa makundi maalum ikiwamo yatima.

"Kuna ombwe kati ya wahitimu na mahitaji ya soko, hali inayosababisha washindwe kushindana kwenye soko, hivyo ni matumaini yetu kuwa mafunzo ni muhimu kuongeza thamani ya wahitimu hawa sokoni," alisema Kiwanga.

Kadhalika, Kiwanga aliongeza kuwa mafunzo hayo yanawajengea uwezo wahitimu wenye nia ya kujiari, ikiwamo kuanzisha biashara

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, uwezo huo utawezesha vijana kutumia fursa iliyopo katika soko na kuharakisha maendeleo kiuchumi.

Mshauri wa Wanafunzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Ulingeta Mbamba, alisema lipo tatizo la ajira wanalokumbana nalo wahitimu wanapotafuta ajira.

Alisema chuo kimeamua kuja na kozi maalum itakayoleta ulinganifu ili kuondoa tatizo hilo.

"Tuna kituo atamizi ambacho lengo lake ni kuwawezesha walio na mawazo ya kibiashara kufikia ndoto zao, chuo kinayaboresha mawazo yao kuwa biashara," alisema Prof. Mbamba.

Sia Ngowa, mwanafunzi wa chuo hicho Taasisi ya Taaluma na Maendeleo (IDS), alisema mafunzo hayo yataongeza ujuzi na kukabiliana na ushindani kwenye soko la ajira.

"Tumepata ujuzi ambao umetufungua kujua ukweli uliopo kwenye soko la ajira nchini na mataifa jirani," alisema Sia.

# Wapania kuenzi maoni, kujenga shule nchi jirani

**Na Enock Charles**

KATIKA kuenzi juhudi za Askofu Getrude Rwakatare, wa Kanisa la Mlima wa Moto, uongozi wa shule za msingi na sekondari za St.Mary's, imetangaza mpango wa kujenga shule kwenye mataifa jirani.

Akizungumza katika mahafali ya wanafunzi 95 wa awali yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa shule hizo, Rose Rwakatare ambaye ni mtoto wa marehemu Getrude Rwakatare, alisema mama yao alikuwa na maono mengi kwa ajili ya wananchi wa Tanzania na wengine wa mataifa jirani na lengo kubwa likiwa ni kuondokana na umasikini na ujinga.

"Kama familia tunatakiwa kuendeleza maono yake na hata yale ambayo hakuyatimiza tunataka tufanye vizuri zaidi ili kule aliko ajivunie alikuwa na maono mengi kwa ajili ya Watanzania hasa wanawake na watoto"

"Tuna mipango za kwenda nchi za nje hasa Msumbiji ambako hawazungumzi Kiingereza wala Kiswahili kwa hiyo tunataka tukajikite huko ili na wao wapate elimu angalau ya Kiswahili na Kiingereza" alisema Rose.

Ofisa Elimu wa Manispaa ya Kinondoni, Martha Kusaga, akizungumza katika mahafali hayo alisema shule za St.Mary's ni mojawapo ya shule zinazofanya juhudi kubwa ya kusomesha hapa nchini na hivyo kuwa msaada mkubwa kwa taifa na kuutaka uongozi wa shule hiyo kuendelee kulinda heshima ya shule hizo kama ilivyoasisiwa na marehemu Dk.Rwakatare

Aliwataka wazazi kuendelea kuwekeza katika elimu ya msingi kwa watoto ili kuwajengea msingi bora kwa maisha ya baadaye na kujiwekea akiba ya uzeeni kwa kuwasomesha watoto katika shule bora na zenye maadili.




Meneja wa kiwanda cha kutengeneza Bia cha TBL Plc Arusha, Joseph Mwaikasu (kushoto) na Meneja Mawasiliano wa kampuni hiyo, Amanda Walter (kulia),wakimkabidhi fulana za uhamasishaji, Ofisa Tawala wa Wilaya ya Monduli, Tateni Malaki, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia zilizofanyika wilayani humo ambapo kampuni ya TBL imeshiriki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasichana waelekezwa kuripoti TAKUKURU rushwa ya ngono

**Sabato Kasika**

WASICHANA walio katika hatari ya kukumbwa na rushwa ya ngono, wametakiwa kutoa taarifa katika mamlaka husika, ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili iwekwe mtego na kuwanasa wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Hayo yalisemwa Dar es Salaam juzi, na Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma wa TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni, Rose Mayala, wakati akichangia mada kwenye mkutano wa tathmini ya kampeni za rushwa ya ngono kwa wanafunzi na wasichana, ziitwazo 'Safari salama bila rushwa ya ngono'.

Mkutano huo uliandaliwa na asasi ya kiraia ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) na kushirikisha wadau wakiwamo walimu, madereva wa bodaboda, bajaj na daladala.

Wengine ni viongozi wa dini, maofisa wa ustawi wa jamii na wazazi, ambapo alisema, rushwa ya ngono imekuwa ikifanyika sirini, hivyo ili kuwanasa wahusika, ni vyema wanafunzi na wasichana wakatoa taarifa.

"Wasichana wakitoa taarifa ni rahisi sisi kuandaa mtego wa kuwanasa watuhumiwa ili tukomeshe vitendo hivyo katika jamii, kwani vinaua na vinadhalilisha utu wa mwanamke," alisema Mayala.

Mayala alisema, mambo hayo ya rushwa ya ngono yanafanyika sirini, na kwamba jambo la muhimu ni wahusika kutoa taarifa kuliko kukaa kimya na kusababisha vitendo hivyo kuendelea kwenye jamii. Alisema si sahihi watu kutumia nafasi zao kuingiza wanafunzi na wasichana kwenye rushwa ya ngono, na kwamba taasisi hiyo haitakuwa tayari kuona mambo hayo kwenye Mkoa wa Kinondoni.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, alisema, vita ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi na wasichana aliianza tangu mwaka 2018 kwa kushirikisha baadhi ya madereva wa bodaboda na daladala. "Tulifanya hivyo, kwa sababu hao ndiyo walikuwa watuhumiwa wakubwa wa kurubuni wanafunzi kwa lifti, na kuna mafanikio, kutokana na kwamba baadhi yao sasa ni mabalozi wa vita ya rushwa ya ngono," alisema Mawinza.

Mshauri wa Kitaalam, Mfuko wa Wanawake Tanzania (Women Fund Tanzania Trust), Dk. Dinah Mmbaga, alisema, vita hiyo wasiachiwe watu wachache bali ni ya jamii nzima.

"Sote tushirikiane kutokomeza rushwa ya ngono kwa wanafunzi na mambo mengine yanayosababisha mmomonyoko wa maadili ili watoto wetu wawe salama zaidi," alisema Dk. Mmbaga.

Alisema, vita hiyo isiishie kwenye rushwa ya ngono, bali hata wale wanaotukana wanawake matusi ya nguoni, nao waelimishwe ili waachane na tabia hiyo ambayo inamomonyoa maadili katika jamii.

# HKMU yaja na machapisho tiba ya malaria

**Na Joseph Mwendapole**

WATAALAMU wa Chuo cha cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), wamefanya utafiti na kutoa machapisho kuhusu njia mpya ya kutibu malaria na magonjwa yanayowakumba watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Makamu Mkuu wa huo hicho, Prof. Charles Mgone, wakati wa mahafali ya 18 ya chuo hicho, ambapo wahitimu 146 walitunukiwa Stashahada ya uuguzi, 53 Shahada ya uuguzi, 183 Shahada ya udaktari wa binadamu na wawili Shahada ya uzamivu ya udaktari wa binadamu. Prof. Mgone alisema utafiti unaendelea kufanywa na wanataaluma wa chuo na wanafunzi wake wa ngazi zote zingine zikihusu magonjwa ya kuambukizwa na yale yasiyo ya kuambukizwa.

Alisema kwa mwaka 2020 baadhi ya wataalamu wa chuo hicho wametoa machapisho kadhaa katika majarida ya kisayansi yakiwamo ya uchambuzi yakinifu kuhusu elimu ya uuguzi na ukunga nchini na utafiti kuhusu njia mpya za kutibu maralia.

Alitaja machapisho mengine ni kuhusu uhusiano kati ya ugonjwa wa seli mundu na malaria, dalili za mwanzo za kuelekea kupata ugonjwa wa kisukari na aina ya magonjwa yanayowasibu watoto wachanga waliozaliwa kabla ya wakati.

Kadhalika alisema HKMU kimeendelea na mpango wake wa kufadhili masomo ya wafanyakazi wake kwa ngazi ya uzamili na uzamivu ndani na nje ya nchi.

Alisema wahadhiri wanne wamemaliza mafunzo yao ya uzamili hivi karibuni akiwamo Dk. Fulgence Mpenda, Dk. Jane Nyandele, Dk. Hosiana Msechu na Dk. Zahra Moraweji.

Prof. Mgone alisema kwa sasa chuo hicho kina wahadhiri 15 wanaosomea shahada ya uzamivu na saba shahada ya uzamili katika fani mbalimbali huku wahadhiri sita wakipandishwa vyeo katika fani mbalimbali.

Alisema katika kuboresha ufundishaji chuo kimeajiri wafanyakazi wapya ili kuendana na ongezeko la wanafunzi na tangu Desemba, 2019 mpaka Novemba, mwaka huu chuo kimeajiri wafanyakazi wapya nane.

# EABL yateua wakurugenzi

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya wakurugenzi wa Kampuni ya Bia Africa Mashariki (EABL), imemtangaza Jane Karuku kuwa mkurugenzi mpya wa kampuni hiyo inayomiliki Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Kampuni ya Bia ya Uganda (UBL) na Kampuni ya Bia ya Kenya (KBL)

Taarifa ya EABL ilieleza kuwa Jane ambaye alikuwa ni mjumbe wa bodi ya EABL na mkurugenzi mtendaji wa KBL, anachukua nafasi ya Andrew Cowan ambaye amekuwa mkurugenzi mtendaji wa EABL kwa miaka minne na nusu. Cowan anakwenda kuchukua nafasi katika kampuni mama ya Diageo akiwa kama mkurugenzi mtendaji wa masoko ya Afrika.

Jane ni kiongozi mahiri wa biashara mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 25. Kabla ya kujiunga na KBL, alikuwa ni rais wa asasi ya kimataifa isiyo ya kiserikali inayojulikana kama Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA) inayohusika na kuratibu ruzuku kutoka kwa mashirika makubwa yanayotoa ruzuku kwenye eneo la usalama wa chakula na maendeleo ya kilimo.

Jane pia ameshika nyadhifa mbalimbali kwenye mashirika tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na Cadbury's East & Central Africa ambapo alikuwa ni mkurugenzi mtendaji ikiwa ni kabla ya kujiunga na Telkom Kenya kama naibu afisa mtendaji mkuu na katibu mkuu. Akiwa Cadbury alikuwa akihusika na nchi 14 zilizopo Afrika

Pia amefanya kazi katika bodi mbalimbali kama Barclays Kenya na kwa sasa ni mjumbe wa shirika la Precious Sisters linalowasaidia wasichana wenye vipaji na wanaotoka katika mazingira magumu kupata elimu. Kwa sasa pia ni mwenyekiti wa mpango wa Kenya Vision 20230 na pia aliongoza bodi ya kupambana na Covid-19 iliyoundwa na Rais Uhuru Kenyata wa Kenya.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa nafasi yake itachukuliwa na John Musunga ambaye atakuwa mkurugenzi mtendaji mpya wa KBL. Musunga ana uzoefu wa zaidi ya miaka 25 kwenye utawala, mauzo na masoko. Anajiunga na EABL kutoka GlaxoSmithKline (GSK)

Musunga amefanya kazi katika bodi mbalimbali na kwa nyadhifa tofauti. Amefanya kazi kama mjumbe wa bodi ya Kenya Vision 2030, mwenyekiti wa Kenya Association of Pharmaceuticals Industry na pia amefanya kazi kama mwenyekiti wa baraza la kibishara la HIV/AIDS.

Taarifa hiyo ilisema uteuzi wa Jane na Cowan utaanza Januari 1, 2021 wakati wa Musunga utaanza rasmi Machi 2021. Cowana ataendelea kuwa mjumbe wa bodi ya EABL.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 6 WALIOKOSA PENALTI LIGI KUU BARA UK. 12-13



MARCELO

# NYOTA WA5 MADRID WANAOWEZA KUSEPA

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imeanza msimu mpya kwa kasi ndogo, ingawa timu nyingine nazo zimekuwa na mwanzo mbaya zaidi msimu huu. Barcelona kwa sasa ipo nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi (kabla mechi za mwishoni mwa wiki). Wapinzani wao wa jiji moja na jirani zao, Atletico Madrid, wapo kileleni mwa msimamo wa LaLiga.

Kuna wachezaji kadhaa ambao wanaonekana kwamba majaliwa yao hayapo tena pale Santiago Bernabeu.

Makala haya yanawatazama wachezaji watano ambao wana uwezekano mkubwa wa kuondoka Real Madrid haraka iwezekanavyo, sasa wafahamu...

### #5. Luka Jovic

Si vigumu kuelewa namna gani mashabiki wa Real Madrid kile wanachokipitia wakati mchezaji wao mwenye uwezo wa kufunga mabao 30 hadi 40 kwenye ligi kila msimu, akishindwa kufikisha hata matatu.

Baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kule Eintracht Frankfurt, Jovic alihusishwa na klabu kadhaa kubwa za Ulaya na Real Madrid wakafanikiwa kupata saini yake.

Hata hivyo, Jovic akawa tena tatizo lingine kwani ameshindwa kukifanya kile alichokifanya wakati akiwa Ujerumani. Alifunga mabao mawili tu katika msimu wake wa kwanza kwenye LaLiga.

Jovic haonekani kuwa kwenye mipango ya muda mrefu pale Real Madrid, kwani nyota huyo aliyenunuliwa kwa euro milioni 50, anaweza akaondoka wakati wowote.

### #4. Mariano Diaz

Ni jambo la kushangaza kuona kwamba, Real Madrid waliamini kwamba kumpa nafasi ya pili Mariano Diaz kucheza tena pale Santiago Bernabeu kungewanufaisha wao. Diaz aliondoka Real Madrid baada ya kuwa na wakati mbaya mwaka 2017.

Alikwenda Olympique Lyon na akafunga mabao 21 katika mechi 48 na Real Madrid wakamtwangia simu na kumnunua kwa euro milioni 21.

Diaz hajawa kwenye ubora wake wa kumuwezesha kuwa mfungaji muhimu wa Real Madrid. Huku mkataba wake ukiwa umebakiwa na miaka mitatu, anaweza kuifanya Real Madrid ipate fedha nyingi kwa kumuuza.

### #3. Alvaro Odriozola

Usajili mwingine wa hivi karibuni pale Real Madrid ambao ulitarajiwa kuwa bora, lakini mambo yakawa tofauti kabisa. Mchezaji huyo wa zamani wa Real Sociedad alisajiliwa kwa euro milioni 30 kipindi cha majira ya joto mwaka 2018.

Amekuwa na wakati mgumu chini ya Zinedine Zidane kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita. Baada ya kuanza katika mechi nne tu za ligi tangu kipindi cha majira ya baridi msimu wa 2019-20, Odriozola alipelekwa Bayern Munich kwa mkopo wakati wa dirisha dogo la Januari.

Amerudi tena Real Madrid, lakini Zinedine Zidane haonekani kama anamhitaji. Zizou amekuwa akimtumia zaidi Lucas Vazquez kuliko Odriozola na msaidizi wake Dani Carvajal. Odriozola ana umri wa miaka 24, hivyo bado anaweza kwenda kutafuta timu sehemu nyingine.

Klabu hiyo imeshafikia mpango wa kuachana mazima na mchezaji huyo wakati wowote kuanzia sasa.

### #2. Marcelo

Marcelo ameitumikia klabu hiyo kwa kipindi kirefu na amekuwa na muda wa kuvutia pale Real Madrid. Amekuwa mmoja wa wachezaji waliowasaidia zaidi 'Los Blancos' hao kutawala Ulaya.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, anaonekana kiwango chake kinazidi kushuka kila siku. Real Madrid imeshinda mechi moja tu kati ya tano zilizopita wakati Marcelo akianza. Bila shaka, lawama si za Marcelo.

Lakini sasa inawezekana Real Madrid wakaona kwamba mpango wa kumuuza Sergio Reguilon haukuwa wa busara kipindi cha majira ya joto. Mkataba wa sasa wa Marcelo unamalizika mwaka 2022. Na huku madirisha mawili ya usajili yanakuja, hivyo Real Madrid wanaweza kuangalia uwezekano wa kumuuza raia huyo wa Brazil ili kupata fedha.

### #1. Isco

Kwa sasa, kila moja anajua kwamba, Isco anatakiwa kuondoka Real Madrid na anatakiwa kufanya haraka zaidi. Ni wazi kwamba hayupo kabisa kwenye mipango ya Zinedine Zidane na amekuwa hana namba kwa miaka ya hivi karibuni.

Mara nyingi anacheza akitokea benchi na Real Madrid inaonekana wazi kwamba haina tena mpango na mchezaji huyo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, anawaniwa na timu kadhaa Ulaya, huku Carlo Ancelotti akitaka kuungana naye.

Isco ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi na kumuuza yeye kutaifanya Real Madrid kuwa vizuri kwenye mipango ya kifedha.

## ISIKUPITE

RAHEEM Sterling ameongeza idadi ya mechi alizocheza dhidi ya Manchester United bila kufunga bao na kuwa 17 kwenye Ligi Kuu England, zikiwa ni mechi 10 zaidi ya alizokutana na timu nyingine za ligi hiyo na kumalizika bila ya yeye kufunga.



# MAKIPA 10 WENYE MECHI NYINGI BILA KURUHUSU BAO MSIMU 2020/21



EDOUARD MENDY

**LONDON,** England

MAGOLIKIPA wanajulikana kama ndio wanaolinda zaidi goli, kwa sababu makosa yao mara zote yanasababisha wao kuadhibiwa. Kwa sababu hiyo, timu kubwa duniani zinahitaji kuwa na magolikipa wenye uwezo mkubwa.

**Na timu hizo zinakuwa na mafanikio makubwa kwa sababu ya uwapo wa kiwango cha juu zaidi.**

Msimu uliopita Real Madrid walitwaa taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, shukrani kubwa kwa safu yake ya ulinzi pamoja na golikipa. Los Blancos hao waliruhusu mabao machache tu (25), huku shukrani kubwa zikienda kwa golikipa wao, Thibaut Courtois raia wa Ubelgiji, ambaye hakuruhusu nyavu zake kutikiswa mara 18.

Nchini Italia, Samir Handanovic hakuruhusu nyavu zake kutikiswa katika mechi 13 na akaisaidia Inter Milan kuwa na msimu mzuri uliopita, huku msimu huu Gianluigi Donnarumma amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi kwa AC Milan kwenye Serie A.

Washindi wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich (wameruhusu mabao 13 tu) yakiwa machache zaidi msimu huu. Hata hivyo, miamba hao wa Bavaria wana mmoja wa golikipa bora duniani, Manuel Neuer.

Kwenye makala haya tunawaangalia magolikipa 10 ambao wamecheza mechi nyingi zaidi bila kuruhusu bao msimu huu nao ni hawa hapa...

### #10. KOEN CASTEELS (WOLFSBURG) - 5 KATI YA MECHI 10

Koen Casteels amekuwa akicheza mara kwa mara kwa kikosi cha Wolfsburg tangu kipa huyo alipotua kwenye klabu hiyo ya Bundesliga kipindi cha majira ya joto mwaka 2015.

Golikipa huyo mwenye mwenye umri wa miaka 28 raia wa Ubelgiji, ambaye alianza kucheza soka la kulipwa katika Klabu ya Genk zaidi ya muongo mmoja uliopita, amecheza mechi 49 bila kuruhu bao katika mechi zaidi ya 150 kwenye mashindano yote kwa Wolfsburg.

### #9. EDERSON (MANCHESTER CITY) - 6 KATI YA MECHI 13

Golikipa wa Brazil, Ederson, amekuwa nguzo kubwa kwa Manchester City tangu alipowasili chini ya kocha Pep Guardiola kipindi cha majira ya joto mwaka 2017.

Nyota huyo wa zamani wa Benfica alicheza mechi 20 bila kuruhusu bao kwa misimu miwili mfululizo na kuiwezesha Manchester City kushinda taji la Ligi Kuu.

Licha ya Man City kukabiliwa na kipindi kigumu msimu huu, golikipa huyo raia wa Brazil amecheza mechi tatu bila kuruhusu bao kwenye Ligi Kuu. Hata hivyo, Ederson amekuwa na wakati wa kuvutia zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo ameruhusu bao moja tu katika mechi tano.

### #8. ROMAN BURKI (BORUSSIA DORTMUND) - 6 KATI YA MECHI 10

Roman Burki amekuwa na kiwango cha kuvutia tangu alipowasili pale Borussia Dortmund katika kipindi cha majira ya joto mwaka 2015.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Uswisi, ambaye amekuwa na wakati wa kuvutia zaidi kwa kucheza mechi 82 bila kuruhusu bao kwenye mashindano yote katika mechi zaidi ya 200 kwa BVB, amekuwa mmoja wa makipa bora zaidi kwenye Bundesliga.

Kiwango chake kimekuwa na msaada mkubwa kwa BVB ambao wanaipa changamoto Bayern Munich kwenye Bundesliga.

Amecheza mechi tatu bila kuruhusu bao kati ya mechi saba za Bundesliga na nne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

### #7. RUI SILVA (GRANADA) - 7 KATI YA MECHI 16

Rui Silva alicheza mechi 12 bila kuruhusu bao kwenye LaLiga msimu uliopita na kuisaidia Granada kumaliza msimamo ikiwa nafasi ya saba kwenye msimamo na kufuzu kwenye Ligi ya Europa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye bado hajaanza kuichezea Ureno, ameendelea na kiwango chake kwenye msimu wa 2020-21. Silva amecheza mechi tatu bila kuruhusu bao kwenye LaLiga na mechi mbili kwenye michuano ya kufuzu kucheza Ligi ya Europa.

Mchezaji huyo wa zamani wa CD National, amecheza mechi 15 bila kuruhusu bao katika mechi 45 kwenye LaLiga na amekuwa nyota wa Granada.

### #6. MIKE MAIGNAN (LILLE) - 7 KATI YA MECHI 16

Mike Maignan amekua na kuimarika kwa kiwango tangu kutua Lille akitokea SG kipindi cha majira ya joto mwaka 2015. Na kipa huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa chaguo la kwanza mara kwa mara katika misimu miwili.

Maginan alicheza mechi sita bila kuruhusu bao katika mechi 34 za ligi msimu huo na kuiwezesha Lille kuepuka kushuka daraja.

Kipa huyo alicheza mechi zote za ligi msimu uliofuata, akiweka rekodi ya kuvutia ya kucheza mechi 15 bila kuruhusu bao wakati wakipambana kutoshuka daraja msimu wa 2017-18.

Maignan aliendelea kuwa na kiwango cha kuvutia kwa msimu wa 2019-20 na kuisaidia timu yake kufuzu michuano ya Ulaya na akawa anawindwa na klabu kama Tottenham Hotspur.

Mfaransa huyo amejijengea heshima kwa kucheza mechi sita bila kuruhusu bao kati ya 12 kwenye Ligue 1 msimu huu na moja kwenye Ligi ya Europa.

### #5. BENOIT COSTIL (BORDEAUX) - 7 KATI YA MECHI 12

Baada ya kuwasili kutoka Stade Rennais mwanzoni mwa msimu wa 2017-18, Benoit Costil amekuwa na namba ya kudumu pale Bordeaux.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 33, amekosa mechi tatu tu za ligi kwa kipindi cha misimu mitatu iliyopita, akijiwekea rekodi ya kucheza mechi 31 bila kuruhusu bao kwenye Ligue 1 kwa kipindi hicho.

Costil amekuwa na kiwango kizuri kwani ana jumla ya mechi 94 alizocheza kwenye Ligue 1 bila kuruhusu bao kati ya zaidi ya mechi 300 kwenye mashindano yote katika klabu tatu tofauti.

### #4. ALEX REMIRO (REAL SOCIEDAD) - 8 KATI YA MECHI 14

Alex Remiro amecheza mechi sita bila kuruhusu bao (katika mechi 25) kwenye LaLiga msimu uliopita.

Remiro alianza kucheza mechi yake bila kuruhusu bao dhidi ya bingwa mtetezi Real Madrid.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, amezidi kuimarika zaidi na kuiwezesha Sociedad kuwapiku miamba ya LaLiga kama Real Madrid, Barcelona na Atletico Madrid, ikiwa kileleni.

### #3. JAN OBLAK (ATLETICO MADRID) - 8 KATI YA MECHI 13

Golikipa huyu wa Atletico Madrid, Jan Oblak amekuwa mmoja wa watu muhimu zaidi kwenye kikosi cha Diego Simeone tangu alipowasili akitokea Benfica miaka sita iliyopita.

Raia huyo wa Slovenia mwenye umri wa miaka 27, ni mmoja wa magolikipa bora kwenye LaLiga na amekuwa nguzo kubwa kwa Rojiblancos hao.

Oblak amecheza mechi 20 bila kuruhusu bao kwenye LaLiga kwa kipindi cha misimu mitatu kati ya sita klabuni hapo. Hata hivyo, msimu huu kipa huyo wa Atletico ameimarika zaidi.

Ni mmoja wa wanaoanza mara kwa mara msimu huu, na ameiwezesha Atletico Madrid iliyopo nafasi ya pili kucheza mechi tisa za LaLiga bila kuruhusu bao, shukrani kwa uwezo wake.

Hata hivyo, kwenye Ligi ya Mabingwa, kipa huyo amecheza mechi moja bila kuruhusu bao kati ya mechi tano.

### #2. KEYLOR NAVAS (PSG) - 8 KATI YA MECHI 12

Baada ya kushinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid, Keylor Navas aliwasili PSG msimu uliopita.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Costa Rica, amecheza mechi 11 bila kuruhusu bao katika msimu wa 2019-20 kwenye Ligue 1 na kuisaidia klabu hiyo ya Ufaransa kutetea taji lake la ligi.

Hata kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kipa huyo wa PSG pia amekuwa na kiwango bora kabisa, akicheza mechi tano kati ya tisa bila kuruhusu bao, kabla ya kushindwa kutwaa taji hilo kwa mara ya nne kwa kipindi cha miaka mitano, baada ya kufungwa kwenye fainali na Bayern Munich.

Navas anaonekana kuendelea pale alipoishia msimu uliopita, akiruhusu bao kwenye mechi mbili tu kati ya nane za ligi kwa PSG. Pia ana mechi mbili ambazo hajafungwa kwenye Ligi ya Mabingwa msimu huu.

### #1. EDOUARD MENDY (CHELSEA) - 9 KATI YA MECHI 12

Edouard Mendy ndio kwanza ametua pale Chelsea kipindi cha majira ya joto akitokea Chelsea majira ya joto.

Raia huyo wa Senegal mwenye umri wa miaka 28, amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kule Chelsea, akicheza mechi tano bila kuruhusu bao na nne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiwango cha Mendy ndicho kimemfanya Kepa Arrizabalaga kupoteza ubora wake, na vijana hao wa kocha Lampard wameonyesha kwamba wao pia wana nafasi kubwa ya kulibeba taji la Ligi Kuu England msimu huu.

## Nukuu

"Cristiano [Ronaldo] ni mashine kamili, mchapakazi ambaye siku zote anataka kuboresha. Lakini kwangu mimi ni kama Messi si binadamu, lakini [Ronaldo] ndiye bora zaidi wa wanadamu," **Beki wa Kati wa Barcelona, Gerard Pique**



"Kama ningeweza kuomba msamaha na kurudi nyuma na kubadilisha historia ningefanya. Lakini goli bado ni goli, Argentina wakawa mabingwa wa dunia na nilikuwa mchezaji bora wa dunia, " **Diego Maradona enzi za uhai wake akizungumzia Goli la Mkono wa Mungu [alilofunga kwa mkono] kwenye Kombe la Dunia dhidi ya England mwaka 1986.**



"Nakumbuka wakati watu wanasema kwamba uwezo wangu umekwisha, nilitwaa mataji matatu ndani ya Manchester United, nilishinda Super Cup na Ligi ya Europa, sasa wananiambia nimechuja, hebu fikiria wapo wengine hawana kabisa haya mataji sasa sijui itakuaje," **Kocha Mkuu wa Tottenham, Jose Mourinho, akitetea mfumo wake wa mashambulizi ya kushtukiza kuwa ni bora kwa kuwa unampa matokeo.**





KASEKE

# WACHEZAJI 6 WALIOKOSA PENALTI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA isingekuwa kukosa penalti Desemba 6, mwaka huu kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting, winga wa Yanga Deus Kaseke angekuwa na mabao manne.

**Jumamosi iliyopita alikuwa mmoja wa wachezaji waliocheka na nyavu kwenye ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Mwadui FC katika Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.**

Kwa sasa ana mabao matatu, na ni mmoja wa wachezaji waliomo kwenye orodha ya wachezaji waliokosa penalti kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Kabla ya mechi za Jumapili, jumla ya penalti 17 zilikuwa zimepatikana kwenye Ligi Kuu, penalti 11 zikitinga wavuni, lakini sita zikiota mbawa, ama kwa kutoka nje, au makipa kuokoa.

Wachezaji ambao wamefunga penalti hizo 11 ni Yusuph Lwenge wa Gwambina, Jabir Aziz wa JKT Tanzania, Salum Kihimbwa wa Mtibwa Sugar, Abdulrazack Mohamed wa Mbeya City, Tuisila Kisinda wa Yanga, Michael Sarpong wa Yanga na Marcel Kaheza wa Polisi Tanzania.

Wengine ni Lenny Kissu wa Biashara United, Richard Mwaikenda wa KMC, Bigirimana Blaise wa Namungo na John Bocco wa Simba.

Hapa ni wachezaji waliokosa penalti kwenye Ligi Kuu, pamoja na mechi husika...

**#1. Yusuph Soka (Coastal Union 0-0 KMC)**

Hii ilikuwa ndiyo penalti ya kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu, ikitolewa Oktoba 14 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, lakini ikikoswa na straika mkongwe Yusuph Soka wa Coastal Union.

Coastal iliyokuwa ugenini ikicheza dhidi ya wenyeji KMC, walibahatika kupata mkwaju wa penalti dakika ya 44, lakini kipa mkongwe na mzoefu, Juma Kaseja aliipangua na kuokolewa na mabeki wa timu hiyo.

**#2. John Bocco (Simba 0-1 Ruvu Shooting)**

Straika wa Simba, John Bocco, aliikosesha timu yake ya Simba angalau kupata sare dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, alipokosa mkwaju wa penati katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ikichezwa Oktoba 26, mwaka huu.

Ilikuwa ni dakika ya 79 wakati Bocco alipopiga mkwaju huo wa penalti, lakini uligonga mwamba wa juu na kurejea uwanjani kabla ya kuokolewa na mabeki wa Ruvu Shooting, mechi ambayo Simba ililala bao 1-0, likifungwa na Fully Maganga dakika ya 35.

**#3. Jacob Massawe (Gwambina 4-3 Mwadui)**

Hii ndiyo penalti inashikilia rekodi ya kuwa ya mapema zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Ilitolewa kwenye sekunde ya 22 na kupigwa dakika ya kwanza na Jacob Massawe wa Gwambina, timu yake ikicheza ugenini dhidi ya Mwadui FC, kwenye Uwanja wa Mwadui Complex.

Penalti yake ilipanguliwa kwa ustadi na kipa wa Mwadui, Mahmood Amir na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

**#4. Lenny Kissu (Biashara United 1-1 Azam)**

Ilikuwa ni burudani ya aina yake kwenye Uwanja wa Karume Musoma wakati Biashara United ilipopata mkwaju wa penalti dakika ya 52 na akapewa Lenny Kissu kwenda kupiga.

Kwenye goli la Azam alikaa David Kissu, kaka wa mpigaji. Hata hivyo, mdogo mtu alishindwa kumfunga kaka yake na mkwaju wake kutoka nje ya lango, mechi ikichezwa Novemba 30, Biashara na Azam zikitoka sare ya bao 1-1 kwa mabao ya Ayoub Lyanga na Timoth Omwenga.

**5. Bigirimana Bleise (Namungo 1-1 Yanga)**

Mrundi Bigirimana Bleise aliikosesha timu ya Namungo bao ambalo lingeweza kuipa timu hiyo ushindi wa mabao 2-1 kama angefunga.

Ni penalti iliyo kwenye rekodi ya kutolewa dakika za mwisho kabisa. Ilikuwa ni dakika ya 90, wakati huo timu hizo zikiwa zimefunga bao 1-1 Novemba 22, mwaka huu, kwa mabao ya Carlos Carlinhos kwa Yanga na Steven Sey wa Namungo.

Penalti hiyo iliokolewa kwa ustadi na kipa Metacha Mnata wa Yanga.

**6. Deus Kaseke (Yanga vs Ruvu Shooting)**

Inaonekana Ruvu Shooting imekuwa na bahati sana kutofungwa mabao ya penalti na timu za Simba na Yanga.

Baada ya Bocco kukosa Oktoba 26, Desemba 26, Deus Kaseke alikosa mkwaju wa penalti wakati Yanga ilipocheza dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, penalti ikipanguliwa na kipa Abdallah Rashid.

Hata hivyo, kwenye mechi hiyo Yanga ilishinda mabao 2-1 yaliyofungwa na Michael Sarpong na la kujifungwa la Cassin Ponera, la Ruvu Shooting likifungwa na David Richard.

## JE, WAJUA?



MANCHESTER United imecheza mechi tatu mfululizo dhidi ya Manchester City bila kuruhusu bao [clean sheets], ikiwa ni mara ya kwanza tangu miamba hiyo ilipohitimisha kukutana mara nne bila kuruhusu bao Oktoba 1995.



# Wahadhiri washauriwa kuwa wabunifu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAHADHIRI wa vyuo vikuu nchini wametakiwa kuwa wabunifu katika ufundishaji kwa kuwapatia mbinu sahihi wanafunzi ili kuwa na uwezo wa kujitegemea katika maisha.

Hayo yalielezwa juzi na Meya wa Jiji la Dodoma, Profesa Davis Mwamfupe, katika kongamano la wanataaluma lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha St John.

Kongamano hilo lilikuwa na mada iliyohusu mchango wa vyuo vikuu katika kuendeleza teknolojia na kuhamasisha uvumbuzi wa mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo endelevu Tanzania.

Mbali na kongamao hilo, pia chuo hicho kilitoa zawadi na cheti kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika ngazi ya Astashahada, Stashaha na Shahada katika masomo mbalimbali.

Prof. Mwamfupe alisema wahadhiri wanatakiwa kuwa wabunifu katika ufundishaji kwa kubadilisha mbinu na kuachana na ufundishaji wa miaka ya zamani kwa kuzinatia matumizi ya teknolojia.

"Tuna jukumu la kuangalia njia za kufundishia sio wanafunzi wanatoka hapa huko wanapoenda, kila mara wanauliza ametoka wapi huyu. Kubwa wanafunzi wanaiga kwetu sisi walimu tunatakiwa kuwa makini na aina ya ufundishaji huna ubunifu wowote lazima yeye atoke hana kitu," alisema.

Meya huyo ambaye pia amewahi kufundisha Vyuo kadhaa kikiwamo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), alisema ni vizuri wanafunzi wakafundishwa jinsi ya kutumia teknolojia kupata maarifa na siyo kwa ajili ya kufaulu mitihani yao.

"Mwanafunzi kapata jibu, tunatakiwa tuulize sasa hilo jibu kalipataje hapo ndio itatusaidia maana jibu anaweza hata kubahatisha.Hatuwezi kupata mtoto kama tulivyokuwa tukifikiria juzi, jana na leo," alisema.

Mhadhiri wa Chuo hicho Idara ya Kiswahili, Dk. Shadidu Ndossa, alisema kwa sasa teknolojia ipo kila mahali, hivyo vyuo vikuu vinatakiwa kuwa na sauti moja ili kusaidia teknolojia isiharibu mila na desturi katika jamii.

"Mfano kwenye katuni tunatakiwa kuzitengeneza zile zenye mahitaji yetu, muhimu kama vyuo vikuu kuyachuja yale yanayokuja teknolojia ipo kila mahali na sawa hatuwezi kuitenga, lakini lazima tuwe na sauti kwa manufaa ya jamii," alisema Dk. Ndossa.

Alisema asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima, hivyo vyuo vikuu vina wajibu wa kuwasaidia ili kuufikia mnyororo wa thamani kwa kutumia teknolijia kubuni mambo mbalimbali.

"Zaidi ya asilimia 60 ni wakulima changamoto ni jinsi ya kuunganisha mnyororo wa thamani vyuo vikuu tuna wajibu na hili," alisema.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Timoth Simalenga, alisema wamejipanga kuhakikisha chuo kinatoa elimu sahihi, huku akisema kwamba ushauri waliopewa na Prof. Mwamfupe wameupokea na wataufanyia kazi.



Waziri wa Wizara ya Nishati, Dk.Merdadi Kalemani, akizungumza katika kikao kazi na wenyeviti wa bodi pamoja na wakuu wa idara za wizara hiyo ofisini kwake eneo la Mtumba jijini Dodoma mwishoni mwa wiki, ambapo aliiagiza bodi ya TANESCO kuwakatia umeme wateja wote wenye madeni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC awatupia majukumu madiwani, watendaji

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga, amewaagiza madiwani, watendaji wa kata na vijiji, kuhakikisha kuwa wanasimamia mapato ya ndani na nje ili kuiwezesha Halmashauri kuwa na maendeleo.

Aidha, madiwani na watendaji hao wametakiwa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kusimamia miradi yote kwa uaminifu, huku pia wakijiepusha na vitendo vya rushwa katika maeneo yao ya kazi.

Nyamoga, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na madiwani kutoka kata zote zilizopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino baada ya kuapishwa.

Mkuu huyo wa wilaya alisema ana matumaini makubwa pamoja na wananchi waliowachagua kuona wanasimamia kwa uaminifu na uzalendo suala la ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya ndani ili kuleta maendeleo.

"Kamwe serikali haitakubari kufanya kazi na diwani yeyote au mtendaji ambaye eneo lake atakuwa akituhumiwa kwa uongozi wake kuwa mbovu, huku wananchi wakipata shida za kukosa huduma wanazostahili, " alisema.

Akizungumza kwenye kikao hicho cha kwanza cha Baraza la Madiwani, aliwataka madiwani kusimamia wanafunzi wote waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2020, na hakuna mtoto yeyote atakayekosa nafasi ya kusoma kwa kizingiizio chochote.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Keneth Yindi, alisema kuwa madiwani waliochaguliwa kupitia kata zao, watakuwa mabalozi wa kulinda vyanzo vyote vya mapato ya ndani na nje kama ilivyoagizwa na serikali ili kuipandisha kiuchumi Halmashauri hiyo.

Alisema madiwani hao watahakikisha wanashiriki kusimamia miradi hiyo, huku wakishirikiana katika kukomesha suala la rushwa ambalo limekuwa ikiwadidimiza wananchi na serikali.

Jumla ya madiwani 51 walikula kiapo na kuahidi kuwa watahakikisha wanaijengea heshima Halmashauri yao katika utendaji kwa kukusanya mapato ndani na nje kwa kuibua vyanzo vipya, ikiwamo kutatua migogoro inayowahusu wananchi.

# IFM yatakiwa kujikita utafiti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha( IFM), Prof. Emmanuel Mjema, amekitaka chuo hicho kujikita kufanya tafiti ndani na nje ya nchi kwa kutumia wataalamu wake.

Wataalamu hao ni wa wa fani za usimamizi wa fedha, uhasibu na sheria za mifumo ya fedha na teknolojia ili kusaidia serikali katika kukabiliana na biashara ya mitandaoni.

Prof. Mjema alisema hayo juzi katika mahafali ya kwanza ya Shahada ya Uzamili wa Fedha ya chuo hicho kampasi ya Dodoma.

Alisema jukumu la kuwaandaa wahitimu wenye viwango vya kimataifa na kukidhi mahitaji ya soko kwa upana wake ni kazi kubwa, ambayo inahitaji juhudi, ubunifu, umakini na nidhamu ya hali ya juu.

"Ni kazi ambayo ina changamoto nyingi na yenye kuhitaji moyo wa kupenda kujisomea, kufanya tafiti kwa bidii na kutoa Elimu hiyo kwa wengine kwa ufasaha." alisema Prof. Mjema.

Alisema Serikali ina matumaini kwamba chuo hicho kitaendelea kutoa wahitimu wenye uwezo wa kuzalisha ajira ili kuchangia mahitaji ya uchumi wa kati unaoongozwa na sekta ya viwanda, ambao Serikali imeufikia kabla ya mwaka 2025 uliokuwa umepangwa.

Hata hivyo, aliwataka wahitimu kuwa wazalendo na kuitumia elimu waliyoipata katika utendaji.

"Tunapofurahia kuhitimu mafunzo ni vyema tukazingatia kazi kubwa mbele yetu ya kuanza kutekeleza kwa vitendo yale tuliyojifunza darasani... tumeachana na ulimwengu wa nadharia tunaingia katika ulimwengu wa utekelezaji kwa vitendo," alisema.

Awali Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Thadeo Satta, alisema wanafunzi waliotunukiwa vyeti vya Shahada ya Uzamili wa Fedha na Uwekezaji katika mahafari hayo ni 27.

Alisema Kampasi ya Dodoma ilianza kutoa mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamili kwa kutumia madarasa ya Chuo cha Mipango na Maendeleo ya Vijijini, lakini hivi sasa wanawashukuru halmashauri ya jiji kuwapa jengo ambalo wamelikarabati na kuanza kulitumia 2020/21.

Alisema chuo hiko katika mwaka huu wa masomo 2020/21 kwa mara ya kwanza kitaanza kutoa mafunzo ya Astashahada katika taaluma za uhasibu, benki na fedha.

Aliushukuru uongozi wa chuo hiko kuendelea kuwaunga mkono kusaidia kufanikisha mahitaji ya maendeleo ya chuo.







Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, ASP Janeth Masangano (katikati), akizungumza kwa niaba ya Umoja wa Wanawake wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wakati wa kukabidhi misaada ya vitu mbalimbali ikiwamo mashuka, sabuni, mafuta ya kula na kupakaa na juisi ambavyo vimegharimu kiasi cha Sh. 650, 000 kwa wanawake na watoto jana. **PICHA GRACE MWAKALINGA**

# Wasiojua kusoma wala kuandika wafanya maajabu

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

IDADI kubwa ya wanafunzi wa shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya waliokuwa hawajui kusoma na kuandika wamefundishwa na kuweza ndani ya mwezi mmoja.

Wamefanikiwa kupitia mradi wa jifunze, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Shirika la Uwezo Tanzania, Zaida Mgala, taarifa aliyoiwasilisha wakati wa kikao cha kutathmini mradi huo kilichofanyika mji mdogo wa Rujewa wilayani Mbarali.

Alieleza kuwa kwa siku 30 walimu wa shule zilizopo kwenye utekelezaji wa mradi huo wa Jifunze, waliwasaidia watoto waliokuwa hawajui kusoma na kuandika kwa kutengeneza mazingira rafiki na mbinu shirikishi ambazo zimewasaidia kujifunza.

Alisema watoto walijifunza kwenye mazingira rafiki ambayo yaliwavutia kusoma huku walimu wakitumia lugha yenye upendo pamoja na michezo mbalimbali ili wasiwachoshe.

Ziada aliongeza kuwa walimu walipewa mafunzo maalum kwa ajili ya kuwafundisha watoto, wazazi na walezi kushirikishwa kwenye meza za majadiliano na kuhamasika kuchangia chakula ambacho kinamsaidia mtoto katika suala la kujifunza.

"Jitihada hizi zimepunguza utoro, mradi huu umewasaidia kuwapa walimu mbinu za kujifunza kwa vitendo, kushirikiana hakuna kuchapwa wala kugombania madawati bali wanakaa chini, wazazi na walezi wameshiriki kuchangia chakula ili kukaa muda wa ziada kujifunza," alisema Mgala.

Mratibu wa Shirika la Elimisha, Debora Mwanyanje, anasema mradi wa Jifunze ulilenga watoto wasiojua kusoma na kuandika ili kusaidiwa.

Alizitaja miongoni mwa shule zilizonufaika na mradi huo kuwa ni Rujewa , Nsonyanga na Mpakani.

Baadhi ya walimu waliofanya kazi hiyo ya tathmini walisema licha ya uchache wa siku za kuwafundisha watoto wasiojua kusoma na kuandika lakini kumekuwa na mafanikio makubwa.

Mdhibiti Ubora wa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali Teobadina Mjimu, aliwaomba walimu waliopata mafunzo hayo kuwapa mbinu za ufundishaji wenzao ambao hawapo kwenye mradi huo ili waendelee kuwasaidia watoto wa madarasa yote wenye tatizo la kutojua kusoma na kuandika.

# Watumishi ulinzi na usalama wasaidia waathirika, wagonjwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIKA kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, Umoja wa Wanawake Watumishi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya, umetoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya wagonjwa waliopo kwenye hospitali ya wilaya hiyo.

Wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Polisi Janeth Masangano, walikabidhi msaada wenye thamani ya Sh.650, 000 kwa wagonjwa mbalimbali. Akizungumza juzi wakati wa makabidhiano Janeth alisema miongoni mwa bidhaa zilizotolewa ni pamoja na mashuka, sabuni za maji , ndoo za kufanyia usafi, sabuni za kufulia, mafuta ya kupaka, juisi na biskuti.

Alisema msaada huo ni kwa ajili ya wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo wakiwamo waliofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia. "Tumeguswa na yanayowakuta wenzetu ndiyo maana tumeamua kuwasaidia wakati tunaendelea na maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na waathirika wakubwa ni kinamama na watoto. Mbali na kutoa msaada lakini pia tumewapa elimu ya kukabiliana na vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kuviripoti polisi," alisema Janeth. Aliwasisitiza kina mama kuongeza umakini katika malezi ya watoto hususani kipindi hiki cha msimu wa sikukuu ambapo kunaibuka wimbi la wizi wa watoto vilevile vitendo vya ubakaji na ulawiti. Katibu wa umoja huo Yusta Mdegela, alisema wanawake wanapaswa kukemea na kuripoti vitendo vya ukatili wa kijinsia na kutoa taarifa kwenye vyombo vya usalama ili sheria ichukue mkondo wake.

Alisema baadhi ya wanawake huwa waoga kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia yanayofanyika katika familia kwa kuogopa aibu au kuharibu uhusiano uliopo baina ya ndugu.

Akizungumza kwa niaba ya watumishi wa afya, Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali Dk.Azaer Luvanda, aliushukuru umoja huo kuwatembelea wagonjwa pamoja na kutoe elimu kwa wanawake kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia.

# Waliofunzwa Kiingereza wajivunia mafanikio

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAFUNZI wa sekondari wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya wamepongeza mradi wa Access Tanzania, unaogharamiwa na Marekani wakiuelezea kuwa umekuwa na manufaa makubwa kwao na kwa wengine.

Mradi wa Access Tanzania unalenga kusaidia watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu lakini wanafanya vizuri shuleni kuwaendeleza zaidi kwa kuwafunza kwa ufasaha Kiingereza.

Mradi huo wa mwaka mmoja ulianza 2019 na kuhitimishwa Desemba 2020, unaelezwa kuwa na manufaa kwa wanafunzi kwani umeongeza ufaulu katika masomo yao, kuwawezesha kuzungumza na kuandika kwa ufasaha Kiingereza, kujiamini sambamba na kuwafundisha wenzao ambao hawakufikiwa na mradi huo.

Akizungumza jana wakati wa kuhitimu mafunzo hayo ya Access Tanzania, miongoni mwa wanafunzi hao, Hawa Mponda kutoka Sekondari ya Legico, alisema Access Tanzania umemwezesha kuzungumza na kuandika Kiingereza kwa ufasaha na kwamba mbinu alizojifunza zimemuandaa kukidhi mahitaji ya soko la ajira duniani.

"Tunashukuru kwa mradi huo, sisi wachache tulibahatika tumendaliwa vyema tunauweza kuzungumza Kiingereza kwa ufasaha mbele za watu na kwa kujiamini, ufaulu katika masomo yangu umeongezeka kwa kuwa naelewa maswali lakini pia somo la Kiingereza ninapata wastani wa alama A," alisema Hawa. Mwanafunzi mwingine Lukelo Mwakajumba, wa kidato cha pili Sekondari ya Mbeya Day, aliwaomba wadau hao kuendelea na mradi huo kwa shule nyingine hapo mkoani Mbeya ili na wengine wajifunze kuzungumza na kuandika Kiingereza.

Alisema amepata mabadiliko makubwa baada ya kupata mafunzo hayo kwa kuwa ameongeza marafiki wa nchi mbalimbali. Zulfa Shaibu mwanafunzi wa kidato cha tatu Sekondari ya Sangu alisema kuwa mbali na kufundishwa Kiingereza lakini wamejengewa uwezo huhusani mabinti kuwa mabalozi wa kupinga ukatili wa kijinsia.

Alisema kwa sasa ni balozi mzuri kwa wenzake shuleni hapo kuwaelekeza athari za ukatili wa kijinsia na kuwaambia kuwa mwanamke akipata fursa katika eneo lolote anaweza kuwakilisha wenzake na kuzungumzia matatizo ya wenzake. Akizungumzia mradi huo, Mratibu wa Access Tanzania, Elimatamu Mwakilasa, alisema jumla ya wanafunzi 25 walipewa ufadhili wa kujifunza Kiingereza kwa miaka miwili, walifundishwa katika muda wa ziada wa masomo.

Alisema mbali na wanafunzi hao 25 kutoka Mbeya kunufaika , umewafikia wanafunzi zaidi ya wanafunzi 400 nchini na kwamba lengo lao ni kuwafikia wanafunzi 400 katika kila mkoa.





Rashid Abdallah Rashid (kulia), akimpa sahani yenye halua Naibu katibu mkuu wa chama cha ACT Wazalendo Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, katika eneo la Darajani Mjini Unguja ikiwa ni ishara ya pongezi kwa chama hicho kuingia katika Serikali ya umoja wa kitaifa Zanzibar. **RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi awaondoa wasiwasi wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewahakikishia wawekezaji wanaotaka kuja kuekeza Zanzibar kwamba Serikali itawawekea mazingira mazuri.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar alipofanya mazungumzo na mmiliki wa Hoteli ya Park Hyatt Ali kutoka Dubai. Alimueleza muwekezaji huyo kwamba Serikali anayoiongoza itahakikisha inafanya kazi vizuri na wawekezaji sambamba na kuwawekea mazingira bora ya uwekezaji.

Alieleza kuwa kwa upande wa sekta ya utalii ambayo ndio inayochangia zaidi katika pato la taifa, Serikali itahakikisha sekta hiyo inawekewa mazingira bora pamoja na wawekezaji wake. Dk. Mwinyi alieleza kwamba Serikali yake imekusudia kufanya kazi na sekta binafsi na inatambua umuhimu wa sekta hiyo katika kukuza uchumi na kuinua pato la Taifa.

Aliongeza kuwa Serikali itahakikisha inashirikiana vyema na sekta binafsi katika kuinua uchumi wa Zanzibar.

Alieleza sekta binafsi ndio injini ya uchumi, hivyo Serikali itaweka mikakati maalum ya kuhakikisha sekta hiyo inaimarika ili kuleta tija kwa nchi na wananchi wake na kuimarika kwake kutaongeza soko la ajira sambamba na pato la Taifa.

Aidha, alisema umuhimu wa kuimarisha bandari na viwanja vya ndege ili sekta ya utalii, biashara na uwekezaji zizidi kuimarika na kusisitiza kwamba hio ndio azma ya Serikali yake.

"Niwakaribishe wawekezaji, wafanyabishara na wenye viwanda wa ndani na nje ya Zanzibar, mje kuwekeza kutokana na kuwapo fursa nyingi hapa nchini," alisema Dk. Mwinyi.

Naye mmiliki wa Hoteli ya Park Hyatt, Ali Saeed Juma, alisema azma ya Kampuni Park Hyatt ya kuongeza uwekezaji Zanzibar kutokana na kuwapo kwa vivutio kadhaa sambamba na ukarimu na utamaduni wa watu wake.

Alisema kampuni yake yenye makao makuu yake nchini Dubai, lakini ina hoteli kadhaa katika nchi mbalimbali duniani inavutiwa zaidi na Zanzibar kutokana na mazingira yake mazuri ya kitalii ukiwamo Mji Mkongwe.

# 50,000 kufanya mtihani darasa la nne leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI wa darasa la nne wa shule za Serikali na binafsi Zanzibar, leo wanaanza kufanya mitihani yao ya taifa na darasa la sita wataanza Desemba 17.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, alisema kuwa mitihani hiyo itaanza kufanyika kwa wanafunzi wa darasa la nne ambao watafanya kuanzia leo hadi kesho.

Alisema kuwa wanafunzi wa darasa la nne walioandikishwa jumla yao ni 50,217 wakiwamo wasichana 24,688 na wavulana 25,529, idadi ambayo imepungua kwa watahiniwa 5,414 sawa na asilimia 9.73 ya mwaka 2019.

Aidha, alisema wanafunzi wa darasa la sita wao watafanya Desemba 17 hadi 21 mwaka huu na kwamba walioandikishwa ni 34,029 wakiwamo wanawake 17,762 na wanaume 16,267 kukiwa na ongezeko la watahiniwa 1,721 sawa na asilimia 5.33 ikilinganishwa na mwaka jana. Aidha waziri huyo alisema kuwa kwa wanafunzi wa kidato cha pili mitihani yao itaanza rasmi Desemba 22 hadi Desemba 31 mwaka huu na wanafunzi 33,897 ndio walioandikishwa wakiwamo wasichana 18,409 na wavulana 15,488.

Waziri Simai alisema watahiniwa hao wa kidato cha pili kuna upungufu wa watahiniwa 576 sawa na asilimia 1.67 ikilinganishwa na idadi wa watahiniwa walioandikishwa kufanya mtihani mwaka 2019.

Aidha alisema wizara yake imeandaa mazingira mazuri ya ufanyaji wa mitihani kwa watahiniwa wenye uhitaji maalumu kulingana na aina ya ulemavu walionao.

"Watahiniwa wenye uhitaji maalumu wameandaliwa mitihani yao kwa mujibu wa hali ya uhitaji wao ikiwamo hati nundu na kukuza maandishi," alisema Simai. Alisema watu wenye uhitaji maalumu walioandikishwa jumla yao ni 1,244 wakiwamo wa darasa la nne 364, darasa la sita 231 na kidato cha pili ni 649.

Aliwataka wazazi na walezi kuwapa hamasa watoto wao ili kufika katika vituo vyao vya mitihani kwa wakati kwa ajili ya kutumia haki yao ya msingi ya elimu sambamba na kuwaomba madereva kutoa ushirikiano kwa wananfunzi ili kufika shule kwa wakati. Pia waziri huyo aliwasisitiza watahiniwa hao kuacha kufanya udanganyifu na vitendo vyote vinavyokwenda kinyume cha kanuni za mitihani na atakaebainika kwenda kinyume na taratibu hizo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufutiwa kwa matokeo yake.

Naye Madina Mjaka Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu Taaluma wa wizara hiyo, alisema wanafunzi wote wamekuwa wakipewa mafunzo sawa, lakini kwa upande wenye uhitaji maalum watapewa upendeleo maalumu ukilinganisha na wanafunzi wa kawaida.

# NMB kukuza uchumi wa Z'bar kupitia utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB imesema imejipanga na kukusudia kuhakikisha inashirikiana na serikali katika kuona sekta ya utalii inakidhi mahitaji ya uchumi wa taifa hilo ikiwamo kukuza sekta ya utalii ambayo imekuwa tegemeo kubwa la uchumi wake.

Imebainisha kuwa na mtaji wa kutosha na imejitolea kutumia wataalamu wake kuona mfumo wa uendeshaji wa sekta ya utalii kupitia teknolojia ya kisasa ya mawasiliano unakwenda kwa kasi na kuleta matumaini makubwa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja Mkuu Huduma za Biashara Serikalini benki ya NMB, Adelard Mang'ombo, wakati akitoa salamu za benki hiyo wakati wa Mkutano mkuu wa Mwaka wa kampuni za waongoza misafara ya watalii Zanzibar (ZATO) uliofanyika Pwani Mchangani.

Alisema benki hiyo inatambua kuwa uchumi wa Zanzibar unategemea sana shughuli za utalii, ambapo kama benki kubwa nchini imejipanga kuhakikisha uchumi huo unaendelea kukua na kuwaletea wazazibar maendeleo.

" Benki yetu imebahatika kuwa na mtaji mkubwa, kupitia mafanikio haya, tunaona kuna umuhimu wa kuungana na serikali na tumekusudia katika hilo, kuhakikisha tunashiriki na sisi katika kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta ya utalii," alisema Mang'ombo.

Mkuu wa Idara ya Biashara za Kadi benki ya NMB, Philbert Casmir, alisema benki imekusudia kutoa ushirikiano mkubwa kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ili kuhakikisha inasaidia kukusanya mapato na kujenga uchumi.

Alisema benki inaamini kuwa uwezo wake katika kukusanya mapato yanayohusu sekta ya utalii, utasaidia kwa kiasi kikubwa kukusanya mapato na kupelekea kufikia lengo la uchumi wa buluu. Kuhusu uchumi wa buluu, Casmir alisema wamejipanga kushirikiana na serikali kutimiza maono yake kwenye uchumi wa buluu na wamenza kwa vitendo kwa kuzindua jukwaa la biashara linalowezesha wafanyabiashara kufanya miamala kupitia tovuti zao (E-Commerce Platform).

Aidha, alisema wamewezesha matumizi ya kadi za malipo za UnionPay na sasa inakubalika katika kufanyia miamala kwenye mashine za kutolea fedha (ATM) na zile za kufanyia manunuzi (POS) za NMB, lengo likiwa kuleta huduma bora kwa wafanyabiashara waliopo kwenye setka ya utalii.

Akiufungua Mkutano Mkuu huo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alizitaka taasisi zinazojishughulisha na sekta ya utalii nchini kutafuta njia mbadala ya kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika kukuza utalii wa kilimo badala ya kuridhika na utalii wa sasa wa viungo ambao tayari umezoeleka.

# Wazazi watakiwa kutoficha watoto wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

WITO umetolewa kwa wazazi na walezi wanaoishi na watoto wenye ulemavu kutowaficha majumbani bali kusaidia kuwapa matumaini kwa kuhakikisha wanapata elimu.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Ofisa Tarafa wa Kawe Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, Salum Chitale, wakati akizungumza katika sherehe za kuadhimisha siku ya kimataifa ya walemavu ambayo huadhimishwa Desemba 3 ya kila mwaka.

Maadhimisho hayo yaliandaliwa na 'All Inclusive' linalojishughulisha na kuwaendeleza watu wenye ulemavu jijini Dar es Salaam, kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Italia. Mradi huo unatekelezwa na Com. Sol kwa kushirikiana na shirika la Watawa la Ivrea Sisters na wadau.

Kitaifa maadhimisho hayo yalifanyika mkoani Dodoma yakiwa na kauli mbiu isemayo 'Si Kila Ulemavu Unaonekana'. Baadhi ya taasisi pia ziliiadhimisha siku hii katika maeneo tofauti tofauti nchi nzima.

Chitale, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo aliwaasa pia wazazi wa watoto hao kuchangamkia fursa za mikopo katika halmashauri ili kuongeza kipato katika ngazi ya familia na kuwahudumia vema watoto hao.

"Halmashhuri zinatoa fursa za mikopo kwa makundi maalum wakiwamo kinamama, vijana na watu wenye ulemavu, mnapaswa kutumia mikopo hii kuanzisha biashara zitakazowaongezea vipato," alisema Chitale.

Sister Karitas Kaihura kutoka shirika la watawa Ivrea Sisters ambaye pia ni Msimamizi Mkuu Msaidizi wa kituo hicho ambacho kinajumuisha shule pamoja na hospitali, alieleza kuwa licha ya kuwapo wafadhili lakini bado mahitaji ya kuwahudumia watu wenye ulemavu wanaofika kituoni hapo hayatoshelezi ikiwamo chakula lishe, uhaba wa wataalamu wa afya na vifaa tiba vya kufanyia mazoezi.

Sister Karitas alionyesha baadhi ya vitu vilivyotengenezwa na vijana wenye ulemavu na kusema kundi hilo la vijana lina uwezo wa kufanya vitu vikubwa zaidi endapo tu litasimamiwa vema.

Alisema kituo cha Antonia Verna kilichopo Kawe jijini Dar es Salaam ni moja ya vituo vya kuwaangalia watu wenye ulemavu wakiwamo watoto na vijana.

Chausiku Fred, Ofisa Ustawi wa kituo hicho, alisema wimbi la wazazi kuwaficha watoto wenye ulemavu limepungua ambapo katika kituo cha Antonia Verna kuna jumla ya watoto 345.

Ametoa wito kwa jamii hususani mashirika na taasisi zinazojihusisha na watu wenye ulemavu kuzidi kutoa elimu zaidi kwa jamii na kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu ili nao wasiachwe nyuma katika shughuli mbalimbali za maendeleo.



Mkuu wa Huduma za Kibiashara wa Benki ya Absa Tanzania, Pius Makalle, akikabidhi baadhi ya vitu walivyotoa msaada kwa Meneja wa Mahabusu ya Watoto Upanga, Darius Damas (wa tano kushoto), kituoni hapo, jijini Dar es Salaam Jana. Katika hafla hiyo wafanyakazi hao walikabidhi vifaa vya umeme wa sola, jokofu, vyakula na misaada mingine ya kibinadamu vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 6.7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule ya viziwi Dar yakarabatiwa

**Na Beatrice Shayo**

SHULE ya Msingi ya Viziwi ya Buguruni jijini Dar es Salaam imefanyiwa ukarabati wa rangi kwenye madarasa pamoja na kutengenezewa jiko la chakula, ambao umegharimu Sh. milioni 31.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa kampuni ya rangi ya Plascon, Hussein Jamal, wakati wakikabidhi jiko walilolitengeneza kwa gharama ya Sh. milioni tatu.

Jamal alisema ukarabati wa upakaji rangi katika shule hiyo unaendelea na unatarajia kukamilika Januari mwakani na gharama za kupaka madarasa yote na bweni utagharimu Sh. milioni 28.

Alisema moja ya sera yao ni kuhakikisha wanachokipata wanakirudisha kwa jamii, na ndio maana wameamua kufanya maboresho katika shule hiyo ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri.

Jamal alisema wataendelea kuisaidia shule hiyo ili kutatua vikwazo wanavyovipata wanafunzi na walimu ukiwa ni mkakati wa kuongeza ufaulu.

Naye Ofisa Elimu ya Watu wazima Manispaa ya Ilala, Hamis Mlangala, alishukuru kupatiwa msaada huo kwa kuwa shule yao imeboreshwa na kuwa na mazingira bora.

Alisema shule inapokuwa katika mazingira mazuri, inachochea kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Mlangala alisema ni vizuri na wadau wengine kuiga mfano uliofanywa na kampuni hiyo katika kuwasaidia wenye uhitaji.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Yahaya Maftah, alishukuru kwa kitendo cha Jamal kuahidi kuendelea kuisaidia shule hiyo.

Alisema wanakabiliwa na tatizo la vifaa vikiwapo vya kusikilizia sauti kwa wanafunzi pamoja na uchakavu wa miundombinu.

# BancBAC yajikita zaidi maboresho teknolojia kidigitali

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya BancABAC imesema inaendelea kufanya maboresho ya teknolojia ya dijitali ambayo yanalenga kuwanufaisha wateja wake kwa kuzindua programu mbalimbali ikiwamo inayojulikana kama 'Kubwa Lao'

Akizungumza jijini Dar es Salaam na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa wateja wadogo na wakubwa wa BancABC Tanzania, Joyce Malai, alisema wameboresha teknolojia kwa kuruhusu wateja wao kutumia kadi yenye teknolojia ya 3D ambayo ina ulinzi zaidi wakati wa kufanya ununuzi kupitia mtandao.

Malai alisema kwa sasa usalama zaidi umeongezwa kupitia teknolojia hiyo na kwamba itakuwa na uwezo wa kuzuia mtu ambae si mmiliki wa kadi ya viza ya BancABC kuitumia kwa kufanya manunuzi mtandaoni bila ridhaa ya mmiliki.

"Hii teknolojia ni ya kisasa na inatusaidia kumfahamu mtumiaji halali na hivyo kuzuia udukuzi au wizi wa kimtandao,"alisema Malai.

"BancABC Tanzania ndio ya kwanza kuzindua kadi hizi za malipo ya kabla, lengo letu ni kuendelea kuongoza kwenye soko na kuwasaidia wateja wetu kuendelea kufurahia huduma ambayo ni salama, rahisi bila kupoteza muda kwa kufanya malipo kwa njia ya mtandao".

Malai alisema huduma hiyo itasaidia kumuongoza mteja kuhakiki taarifa ili kuthibitisha utambulisho.

Mkuu wa Kitengo cha Kiditali BancABC, Lameck Mushi alisema kuwa kadi za malipo ya kabla za fedha za Tanzania zimeunganishwa na maombi maalum ambayo yatamsaidia mteja kuweka au kutoa pesa kwenye akaunti kwa kutumia simu ya mkononi.

"Kwa sasa, hakuna sababu ya kutembelea tawi lolote la benki kwa ajili ya kufanya muamala wa aina yoyote, mteja anaweza kupata salio la akaunti yake, taarifa za miamala yake akiwa mahali popote na atapokea ujumbe mfupi wa maneno kwa kila muamala unaofanyika,"alisema Mushi.

**Kadi za malipo ya kabla za fedha za Tanzania zimeunganishwa na maombi maalum ambayo yatamsaidia mteja kuweka au kutoa pesa kwenye akaunti kwa kutumia simu ya mkononi.**

# Wanafunzi wavamiwa na wenye silaha, wapotea

**Katsina,** NIGERIA

MAMIA ya wanafunzi wanahofiwa kupotea baada ya watu wenye silaha kuvamia shule ya upili kaskazini magharibi mwa Nigeria.

Washambuliaji walifika eneo hilo na pikipiki na kufyatua risasi hewani na kusababisha watu kukimbia, wakilenga shule hiyo ya sayansi ya serikali yenye wanafunzi zaidi ya 800, mashuhuda walieleza.

Jeshi limesema lilikabiliana kwa risasi na watu wenye bunduki kwenye maficho msituni, indawa maofisa walisema hakuna ripoti za wanafunzi kujeruhiwa.

**Rais Buhari alilaani shambulio hilo na kuamuru shule hiyo ifanyiwe ukaguzi ili kubaini wanafunzi wangapi wanakosekana.**

Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, alilaani shambulio hilo na kuamuru shule hiyo ifanyiwe ukaguzi ili kubaini wanafunzi wangapi wanakosekana.

Wakazi wanaoishi karibu na shule ya bweni ya wavulana katika eneo la Kankara, waliiambia BBC kuwa, walisikia milio ya risasi majira ya saa tano usiku, Ijumaa na kwamba shambulio hilo lilidumu kwa zaidi ya saa moja.

Wafanyikazi wa usalama katika shule hiyo waliwafukuza baadhi ya washambuliaji kabla ya ulinzi kuimarishwa na polisi, maofisa walisema.

Karibu wanafunzi 200 ambao walikuwa wamekimbia awali walikosemana, huku mashuhuda wakisema wanafunzi kadhaa walichukuliwa na watu wenye silaha. **BBC**




Wakazi na wazazi wa wanafunzi waliofika katika eneo la Shule ya Sekondari ya Sayansi ya Serikali yenye wanafunzi zaidi ya 800, baada ya watu wenye silaha kuvamia shule hiyo, iliyopo kaskazini magharibi mwa Nigeria. **PICHA/BBC**

## Mpango maendeleo ya kiuchumi watangazwa

**Gabis,** TUNISIA

SERIKALI ya Tunisia imetangaza mpango wa maendeleo kwa ajili ya kuboresha eneo la Gabis, kufuatia maandamano yaliyoandaliwa na wananchi, kudai hali bora ya kijamii na kiuchumi.

Maelezo rasmi yaliyoandikwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, yaliarifu kuwa serikali imeandaa mpango huo, kuhakikisha ajira kwa wananchi kupitia shughuli za maendeleo katika eneo hilo.

Mpango huo unahusisha maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kiafya, kimazingira, viwanda, nishati, uchukuzi, kilimo na utalii.

Waziri Mkuu Hisham al-Mashishi, tayari amechukua uamuzi wa kutuma timu katika eneo hilo, ili kuharakisha utekelezaji wa mpango huo.

Hata hivyo hakuna maelezo zaidi na ya wazi yaliyotolewa kuhusu namna ya utekelezaji na tarehe kamili ya kuanzisha mpango huo.

Maeneo ya kusini na katikati mwa Tunisia ambayo yamezorota kiuchumi kwa ukosefu wa maendeleo, yamekumbwa na maandamano ya kupinga hatua zilizochukuliwa dhidi ya janga la corona kwa kudhoofisha hali ya maendeleo.

Zaidi ya wiki mbili waandamanaji wamekuwa wakikusanyika na kufunga njia ya kuingia eneo la kemikali la Tunisia na kusababisha uhaba wa gesi katika eneo mjini Gabis. **TRT**

## Marekani kuanza kutoa chanjo ya corona leo

**Washington,** MAREKANI

MAOFISA wa Marekani wamesema chanjo ya virusi vya corona iliyotengenezwa na kampuni mbili za Pfizer na BioNTech, itaanza leo, siku kadhaa tangu matumizi yake yalipoidhinishwa.

Jenerali wa Jeshi la Marekani anayesimamia usambazaji wa chanjo hiyo, Gus Perna, alisema dozi za kwanza zilisafirishwa jana na leo, utoaji chanjo utaanza kwa asilimia 100.

Perna aliarifu kuwa ifikapo vituo vya kutolea chanjo 145 vitakuwa vimepokea shehena ya kwanza, huku vituo 425 vitapelekewa chanjo siku ya kesho na chanjo hiyo itapokelewa pia kwenye vituo vingine 66 siku ya Jumatano.

Kampuni inayotengeneza chanjo hiyo ilisema inafanya kazi na washirika wengine kuanza kusafirisha chanjo kwa kutumia magari ya mizigo kutoka kwenye maghala yake yaliyoko kwenye majimbo Michigan na Wisconsin kwenda majimbo yote 50 ya Marekani. **DW**

# ‘Dharura mabadiliko tabianchi haina chanjo’

**Washington,** MAREKANI

WAKUU wa nchi na serikali 77 wameungana na viongozi wa kampuni za biashara mwishoni mwa wiki, kwa njia ya mtandao kuzungumzia malengo ya mabadiliko ya tabianchi na kuyatimiza.

Katika mkutano huo, viongozi waliweka matarajio makubwa zaidi duniani miongoni mwa serikali, kampuni na asasi za kiraia.

Pia mkutano huo uliadhimisha miaka mitano baada ya makubaliano ya mkutano wa Paris wa mabadiliko ya tabianchi kusaidia kutimiza malengo yaliyowekwa Desemba 12, mwaka 2015.

Picha za video zilionyeshwa kwenye mkutano huo kuhusu hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi duniani, kuanzia kuyeyuka kwa barafu, moto wa msituni, majanga ya asili na kilio cha vijana cha kutaka hatua zichukuliwe.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres ni miongoni mwa washiriki wa mkutano huo akizungumza katika ufunguzi alisema, miaka mitano baada ya mkutano wa Paris, dunia bado haipo katika njia sahihi ya kutimiza malengo.

“Ahadi ya Paris ni kudhibiti kiwango cha joto kusalia nyuzi joto 1.5C lakini ahadi iliyowekwa Paris haitoshi kufikia lengo, hata ahadi hizo hazijatimizwa,”

Viwango vya hewa ukaa hivi sasa viko katika viwango vya juu katika historia, kwani tuko katika nyuzijoto 1.2C juu ya ilivyokuwa kabla mapinduzi ya viwanda.” Katibu Mkuu alisisitiza endapo hakuna mabadiliko mwelekeo utakuwa kwenye kiwango cha joto ambacho ni zahma kikiongezeka kwa zaidi ya nyuzijoto 3C katika karne hii.

Guterres aliongeza kuwa hadi sasa nchi 38 zimeshatangaza dharura ya mabadiliko ya tabianchi na wametambua uharaka na hatari iliyopo.

Katibu Mkuu alisema juhudi za kujikwamua na janga la corona au COVID-19 zinatoa fursa ya kiuchumi na jamii kufuata njia bora ya kuelekea kutimiza malengo ya ajenda ifikapo 2030. **UN**

## Polisi wahukumiwa mauaji mchuuzi

**Cairo,** MISRI

MAHAKAMA moja nchini Misri imewahukumu kifungo cha miaka mitatu maofisa tisa wa polisi kwa kosa la kumtesa na kusababishaa kifo cha mchuuzi wa samaki.

Taarifa hiyo imeelezwa na duru za mahakama nchini humo.

Hukumu hiyo ni hatua isiyo ya kawaida ya maofisa kukabiliwa na mkono wa sheria katika nchi hiyo ambako taasisi za kiusalama aghalabu hutuhumiwa kwa unyanyasaji.

Maofisa hao wa polisi wanaweza kukata rufaa dhidi ya hukumu hiyo kwa mujibu wa taarifa.

Mashirika ya haki za binadamu mara kwa mara yamekuwa yakizishutumu idara za usalama nchini Misri kwa unyanyasaji na utesaji madai ambayo yamekuwa yakipingwa na wizara ya mambo ya ndani nchini humo. **DW**

# KAREMBEU AMTAKA MBAPPE KUAMUA




**PARIS,** Ufaransa

CHRISTIAN Karembeu anasubiri kusikia kama Kylian Mbappe ataongeza mkataba pale Paris Saint-Germain au kuamua kujiunga na Real Madrid.

Huku akiwa amebakiwa na miezi 18 kwenye mkataba wake wa sasa pale Parc des Princes, majaliwa ya Mbappe yanaonekana kuwa kwenye wakati mgumu. PSG wangependa kumuona anabaki na kuendelea kucheza katika timu hiyo kwa kipindi kirefu, lakini Real Madrid nayo inawania saini yake kwa udi na uvumba.

Hata hivyo, inaonyesha wazi kwamba, Madrid wana nafasi kubwa ya kumsajili, baada ya nyota huyo kuonyesha kutaka kupambana na changamoto mpya.

Karembeu, mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 1998, anaamini hakutakuwa na haraka kwa nyota huyo ambaye naye alitwaa Kombe la Dunia mwaka 2018.

"Ni ndoto, lakini tunatakiwa kusubiri," alisema Karembeu.

"Real Madrid ina mashabiki ambao wanasubiri kusikia kuhusu Kylian, lakini kwa sasa tunatakiwa kusubiri," Karembeu aliiambia Stats Perform News.

# Solskjaer: Tulikuwa bora dhidi ya Man City

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesifia kiwango cha Manchester United kwenye mchezo wa 'dabi' ya Jumamosi dhidi ya Manchester City, licha ya kumalizika kwa suluhu pale katika dimba la Old Trafford.

Man United kwenye mchezo huo walionekana kuwa bora zaidi, lakini walishindwa kuzitumia nafasi walizopata kufunga mabao.

United walikuwa kwenye nafasi ya kupata bao la mapema la penalti baada ya Kyle Walker kumdondosha chini Marcus Rashford eneo la hatari, lakini VAR ikaonyesha kwamba, mshambuliaji huyo wa England alikuwa ameotea.

United iliifunga City katika mechi tatu kati ya nne zilizopita, zote zikiwa za Ligi Kuu, lakini Solskjaer aliwasifia wachezaji wake kwa kusahau kutolewa na RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa na kuonyesha kiwango cha kuvutia.

"Kwa kipindi changu dhidi ya Manchester City, mchezo wa leo (juzi) ndio ulikuwa bora zaidi kwa upande wangu.

"Wachezaji walikuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi na walionyesha wanapambana kwa ajili ya timu," alisema akiiambia Sky Sports.

"Ulikuwa mchezo mgumu. Najua kwamba tuliwafunga kwenye mechi za msimu uliopita, lakini leo (juzi) ulikuwa mchezo tofauti kabisa."





# *Zidane apagawa na viungo Madrid*

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anaamini viungo nyota pale Real Madrid wamerudi kwenye kiwango chao bora baada ya kuwa na mchango mkubwa wakati wakishinda kwa mabao 2-0 dhidi ya Atletico Madrid.

Casemiro, Luka Modric na Toni Kroos walianza pamoja kwenye mchezo huo wa LaLiga wa Jumamosi ikiwa ni mara ya tatu msimu huu.

Madrid walianza kuongoza kwa bao la Casemiro na wakapata la pili baada ya golikipa, Jan Oblak kujifunga kipindi cha pili.

Zidane alionyesha kufurahishwa zaidi na kiwango cha Modric na Kroos kwenye mchezo huo.

"Tuliwatumia (Modric na Kroos) kutafuta njia, ni kweli," alisema Zidane, ambaye hajapoteza mechi saba dhidi ya Atletico.

"Tulitakiwa kupambana kwa namna yoyote, na kwa hakika kabisa tulikuwa kwenye kiwango bora kabisa.

"Na baadaye tulicheza kwa kiwango bora zaidi cha kuvutia kwa hakika tulikuwa kwenye nafasi nzuri zaidi."

HABARI MICHEZO

# Pogba: Naipigania Man United

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba amesisitiza mara zote "atapambana" kwa ajili ya Manchester United na kubainisha kwamba anataka kuonyesha ubora wake, licha ya kauli ya hivi karibuni ya wakala wake, Mino Raiola.


Mapema wiki hii, baada ya Man United kutolewa na RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Raiola alinukuliwa na gazeti la Italia, Tuttosport akisema kwamba, muda wa Pogba kukaa klabu hapo "umeisha".

Katika mahojiano kamili, Raiola alielezea na kusisitiza kuwa Pogba hana furaha pale kwenye dimba la Old Trafford na yupo tayari kurudi Juventus.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022, ikiwa na maana kwamba klabu hiyo inatakiwa kukaa naye na kukubaliana kuhusu mkataba mpya.

Pogba alicheza kwa dakika zote 90 wakati Man United ikitoka sare na wapizani wao wa jiji moja, Manchester City, Jumamosi.

Pogba aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram, akisema: "Mara zote nimekuwa napambana kwa ajili ya Manchester United, kwa ajili ya wachezaji wenzangu na mashabiki. Bla bla si muhimu kwangu kwa sasa.





# GUARDIOLA AISHIA KUSIFU 'PIRA BIRIANI'

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesifu kiwango cha timu yake, Manchester City wakati ikitoka suluhu na Manchester United pale kwenye dimba la Old Trafford, Jumamosi.

Safu ya ulinzi ya City ilionekana kucheza kwa bidii zaidi, huku John Stones akionyesha kiwango cha kuvutia.

Guardiola anatambua kwamba, kiwango hicho wanaweza kukitumia kwenye mechi zake nyingine za Ligi Kuu na kupata matokeo mazuri zaidi.

"Hatukupoteza. Msimu uliopita tulipoteza. Tulikuwa na nafasi wakati tulipoweza kukimbia," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports.

"Kwa nafasi yetu kwenye mchezo huo tulikuwa na nafasi ngumu ya kutengeneza mashambulizi kwa sababu wao walikuwa imara zaidi na walikwenda mbele kwa haraka. Na sisi tulitakiwa kuwa makini.

"Tulikuwa na nafasi kipindi cha kwanza, lakini hatukuweza kutumia makosa ya Victor Lindelof.

"Tulitengeneza nafasi nyingi, hasa ukizingatia kwamba tupo kwenye hali gani kwa sasa. Ilikuwa nafasi nzuri zaidi kwetu."

# *Mourinho, Fernandes wang'ara Ligi England*

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, ameshinda tuzo ya kocha bora wa Novemba kwenye Ligi Kuu England.

Mourinho ametwaa tuzo hiyo baada ya kumaliza mwezi bila kupoteza mechi yoyote ya Ligi Kuu England na kuendelea kuongoza usukani wa ligi hiyo.

Mourinho aliiongoza Spurs kushinda 1-0 dhidi ya Brighton na West Brom, kisha kushinda 2-0 dhidi ya Manchester City na suluhu mbele ya Chelsea.

Katika tuzo hiyo amewashinda makocha wenzake, Frank Lampard wa Chelsea, David Moyes wa West Ham na Ole Gunnar Solskjær wa Manchester United.

Wakati huo huo Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa Novemba.

Alifunga mabao manne kwenye Ligi Kuu ndani ya mwezi huo.

Alifunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho dhidi ya Eveton, kisha alifunga katika ushindi dhidi ya West Brom na dhidi ya Southampton.

Amewashinda wachezaji wenzake, Ben Chilwell wa Chelsea, Jack Grealish wa Aston Villa, Pierre-Emile Hojbjerg wa Tottenham, Angelo Ogbonna wa West Ham na James Ward-Prowse wa Southampton.

Bruno ambaye alijiunga na Man United Januari mwaka huu, ndiye mchezaji wa kwanza kubeba tuzo tatu ndani ya mwaka mmoja kwenye Ligi Kuu England tangu Harry Kane alipofanya hivyo mwaka 2017.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LAMPARD SASA AITOA CHELSEA UBINGWA EPL

●●● Huwa nasoma kwamba tuna kikosi imara zadi kwenye ligi, lakini sielewi, tuna wachezaji vijana...

**MANCHESTER,** England

FRANK Lampard hana muda wa kufikiria kwamba, Chelsea wana kikosi imara zaidi kwenye Ligi Kuu England baada ya kufungwa na Everton.

**Bao la Gylfi Sigurdsson la dakika ya 22 kwa mkwaju wa penalti liliifanya Everton kuibuka na ushindi wa 1-0 Jumamosi na kumaliza umwamba wa Chelsea wa kutofungwa mechi 14.**

Wakati wanakaa kwenye nafasi ya tatu katika msimamo, kipigo hicho kilikuwa pigo kubwa kwa Chelsea katika mbio za ubingwa, wakiwa wameachwa pointi mbili na Tottenham na Liverpool, ambao walikuwa wanacheza jana Jumapili.

Wiki iliyopita, vijana hao wa Lampard walitajwa kwamba wana nafasi kubwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu na kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp baada ya kutumia fedha nyingi kwenye usajili, lakini mchezaji huyo wa zamani wa England ametupilia mbali mawazo hayo kwamba ana kikosi imara.

"Huwa nasoma kwamba tuna kikosi imara zadi kwenye ligi, lakini sielewi," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "Kuna vikosi na timu zinazotuzunguka sisi na zimeshinda taji miaka mitatu au minne iliyopita na wana wachezaji ambao huwezi kuwalinganisha na kikosi changu.

"Wana washambuliaji wenye mabao 30, wanafunga mbao 20 au 30 kwa mwaka na wameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Sisi hatuna hilo.

"Tuna wachezaji vijana, baadhi ya vijana ambao wameshinda taji, lakini tuna wachezaji wapya kwenye ligi. Tuna wachezaji ambao wanacheza kwenye Ligi Daraja la Kwanza au kwa mkopo kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita. "Tunaendelea kufanya kazi usiku na mchana kuona nini kitatokea. Sipendi, lakini hiyo ni changamoto kwetu sisi kuhakikisha hilo linatekelezwa, ngoja tuone kitakachotokea Jumanne."

Chelsea walipiga shuti la mwisho lililolenga bao dhidi ya Everton katika dakika ya 28 wakati wakikumbana na kipigo chao cha kwanza kwenye ligi msimu huu.

Reece James na Mason Mount mashuti yao yaligonga mwamba kwenye dimba la Goodison Park, lakini Lampard alikilaumu kikosi chake kwa mwanzo mbaya.

"Nafikiri tungeweza kufanya kitu fulani, lakini siwezi kusema kwamba tulikuwa na bahati mbaya, kwa sababu huo ni mchezo wa soka na sidhani kama watu wanaangalia zaidi nafasi walizozipoteza," alisema.

"Tulikuwa na nafasi ambayo nimeitaja (James na Mount waligonga mwamba), lakini hilo halikufanyi upate pointi. "Tumekuwa kwenye kiwango bora na kwa uhakika kabisa tunacheza vizuri na tunajua kwamba tunaweza kufanya kitu fulani.

"Everton walikuwa wa kawaida kama sisi na walijaribu kutushambulia kipindi cha kwanza.

"Ukiwa nyuma kwa bao 1-0, unajiweka mwenyewe kwenye matatizo na unatakiwa kufanya kitu fulani.

"Mchezo ulikwenda kwa mtindo huo na hatukuwa na nafasi ya kubadilisha matokeo."

Chelsea sasa itacheza na Wolves kesho Jumanne kwenye mchezo mwingine wa Ligi Kuu England.

## ZISIKUPITE

### SZOBOSZLAI NJIAPANDA

KIUNGO wa Red Bull Salzburg, Dominik Szoboszlai mwenye umri wa miaka 20 raia wa Hungary, anapanga kuitosa Arsenal na atajiunga na RB Leipzig dirisha dogo la Januari. ***(Sky Germany via Sky Sports)***

### RODGERS HAMTAKI GRAY

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers amemwabia winga wa kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 21, Demarai Gray, hayupo kwenye mipango ya baadaye ya klabu hiyo. ***(Mail)***

### GREALISH HATIHATI VILLA

DEAN Smith amesema Aston Villa inatakiwa kufikia malengo ya Jack Grealish kucheza Ulaya au kukabiliwa na uwezekano wa kumpoteza nyota huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Birmingham Mail)***

### CAVANI ALIZIKATAA JUVE, INTER

STRAIKA wa Uruguay, Edinson Cavani, mwenye umri wa miaka 33, alikataa ofa za kujiunga na Juventus na Inter Milan na kuamua kutua Manchester United kwa uhamisho huru. ***(Sun)***

### WIKNS KUTETA NA LEVY

KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Harry Winks mwenye umri wa miaka 24, yupo tayari kuzungumza na Mwenyekiti, Daniel Levy, kuhusu majaliwa yake ya baadaye na kwa ajili ya nafasi yake England kwenye michuano inayokuja ya Ulaya. ***(Telegraph)***

### DIAWARA AWANIWA EPL

KLABU za Leicester na West Ham zinamuwania kiungo wa Guinea, Amadou Diawara mwenye umri wa miaka 23, ambaye anaweza kuuzwa na AS Roma. ***(Leicester Mercury)***

### GIROUD ARUDISHWA ARSENAL

STRAIKA wa zamani wa Manchester United, Louis Saha anaamini Arsenal inaweza kufikiria kumsajili tena mshambuliji wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 33 kutoka Chelsea, wakati wa dirisha la Januari. ***(Metro)***

### HUDSON-ODOI HATAKIWI

BAYERN Munich haitamfuata winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi wakati wa dirisha la usajili la Januari, lakini mabingwa hao wa Ulaya wanaendelea kumfuatilia nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, raia wa England. ***(Goal)***

### HAALAND KWENYE RADA

TIMU za Manchester City na Manchester United zote zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili straika wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

### RAPHINHA NA RENNES

WINGA wa Leeds United, Raphinha mwenye umri wa miaka 23, amekubali kwamba alikatishwa tamaa na uamuzi wa Rennes kumuuza yeye kwenda Ligi Kuu England, bila kujua. ***(ESPN Brazil via Goal)***

# Mgosi alia na marefa sare Simba, Yanga

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edina Lema, akisema matokeo ya sare tasa waliyoyapata dhidi ya Simba Queens juzi yametokana na kukijenga kikosi chake kwa kufanya usajili ambao ni mahitaji ya timu yao msimu huu ili kuweza kutoa ushindani, kocha Musa Hassan 'Mgosi' (pichani chini) wa Wadada wa Simba hao, yeye amewageukia marefa.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga Princess kuendelea kutamba kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake, lakini pia ikifuta uteja wa misimu miwili ambapo imekuwa ikiangukia kipigo kutoka kwa Simba Queens kila zinapokutana kwenye ligi hiyo.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Simba Mo Arena, uliopo Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, ulikuwa na ushindani mkali lakini kwa Yanga ikionekana kuimarika zaidi kuliko misimu iliyopita ambayo ilikuwa moja ya timu vibonde.

Lakini Edna akizungumza na Nipashe, alisema matokeo hayo ni baada ya kukijenga kikosi chake pamoja na kufanya usajili ambao ni mahitaji ya timu yao kwa msimu huu kushindana.

"Msimu huu tumedhamiria kufanya vizuri katika ligi hii, kwanza tufute ile dhana ya kufungwa na Simba Queens, hilo tumefanikiwa, lakini pia tunahitaji kupata matokeo mazuri kuelekea lengo letu la ubingwa," alisema Edna.

Naye Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mgosi, amewataka waamuzi kutumia sheria za soka na kuchezesha kwa haki bila kufuata maelekezo na kubeba matokeo yao kichwani.

Alisema wachezaji wake wamekuwa wakichezewa rafu ikiwamo mchezo huo dhidi ya Yanga ambapo nahodha wa Yanga Princess alimpiga teke la



mbavuni Opah Clement na kumsababishia kushindwa kuendelea na mchezo huku akikimbizwa hospitalini kwa gari ya wagonjwa kutokana na kushindwa kupumua vizuri.

"Lakini katika hali ya kushangaza, yule refa katoa kadi ya njano tena baada ya kuona madaktari wametumia muda mrefu kumtibu Opah, vinginevyo alishaoneka-na kutokuwa na mpango wa kutoa kadi.

"Tukio hilo la Opah lilikuwa ni muendelezo wa rafu ambazo nahodha huyo wa Yanga Princess na wenzake walizifanya kwa mchezaji wetu, Mwanahamisi Omary," alilalama Mgosi na kuongeza.

"Dakika chache kabla ya mechi hiyo kumalizika, beki wa kushoto, Dotto Evarist, alishindwa kumaliza mchezo na kukimbizwa hospitali kwa gari ya wagonjwa baada ya kurukiwa kwenye enka, lakini refa hakutoa hata kadi ya njano."

# SIMBA SC KUCHAGUA MWENYEKITI JANUARI

**Na Saada Akida**

KAMATI ya Uchanguzi ya Simba chini ya Mwenyekiti wake, Boniface Lihamwike, imeitangaza Januari 7, mwakani kuwa tarehe rasmi ya kufanyika uchanguzi mdogo wa kuziba nafasi ya mwenyekiti.

**Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Lihamwike alisema kuwa, wameanza mchakato wa uchanguzi mdogo wa kuziba nafasi ya Sued Mkwabi ambaye alijiuzulu katika nafasi hiyo kutokana na sababu zake binafsi.**

Alisema lengo la uchaguzi huo ni kutoa nafasi kwa wanachama kupata kiongozi ambaye atawawakilisha katika vikao vya bodi ya wakurugezi kwa ajili ya maendeleo ya klabu ya Simba.

"Uchaguzi huo utakuwa huru na haki, mwanachama yeyote ambaye ana kigezo cha kugombea anatakiwa kuchukua fomu, kutokana na ibara ya 27 ya Katiba ya Simba, mgombea anatakiwa kuwa na elimu ya shahada ya kwanza inayotambulika na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), lazima pia awe na kadi ya uwanachama ambayo ni hai," alisema Lihamwike.

Naye Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Steven Ali, alisema mchakato huo wa uchanguzi unaanza leo kwa wagombea kuchukuwa fomu ambazo zitatolewa Makao Makuu ya klabu hiyo Msimbazi jijini Dar es Salaam.

Alisema mchakato wa kuchukuwa na kurudisha fomu utaendelea hadi Desemba 24, ambayo itakuwa siku ya mwisho na kuanzia Desemba 27 hadi 28, mwaka huu fomu hizo zitapitiwa na kufanya usaili.

"Kuanzia Desemba 29, majina ya wagombea yatawekwa hadharani hadi Januari Mosi, baada ya hapo Januari 2, mwakani tutapokea na kupitia mapingamizi.

Januari 3, mwakani tutasikiliza na kutolea uamuzi mapingamizi, baada ya hapo tutangaza majina rasmi ya wagombea ambao wamepita mchakato huo," alisema Steven.

Alisema kuanzia Januari 5-6, ni kipindi cha kampeni kwa wagombea hao na Januari 7, mwakani, itakuwa siku rasmi ya uchaguzi.

**YAKO HII...**



Msanii wa vichekesho, Lucas Mhavile maarufu Joti (kulia), akimkabidhi zawadi ya simu aina ya Samsung note 20, mshindi wa Kampeni ya Jaza Tukujaze Tena, Habiba Ali, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kasulu Uvinza Combine mabingwa Lake Tanganyika Cup

**Na Pendo Thomas,** BURUNDI

TIMU ya soka ya Mkoa wa Kigoma, Kombaini ya Kasulu Uvinza, imetwaa Kombe la Lake Tanganyika baada ya kuifunga mabao 2-0 timu pinzani ya Academy ya Mkoa wa Ruyigi, Burundi katika mechi ya fainali.

Michuano hiyo iliyofanyika kwenye Uwanja wa Nkurunzinza Peace Complex uliopo Mkoa wa Makamba nchini Burundi kuanzia Desemba 6, mwaka huu kabla ya mechi hiyo ya fainali kupigwa Jumamosi iliyopita na timu hiyo ya Tanzania kuibuka mabingwa, ilishirikisha jumla ya timu nane.

Timu hiyo ya Kombaini ya Kasulu Uvinza, ilikuwa moja kati ya nne kutoka Mkoa wa Kigoma ambazo zilishiriki michuano hiyo iliyoshirikisha timu nyingine nne kutoka Burundi.

Akifunga michuano hiyo na kukabidhi zawadi kwa mabingwa, Naibu Spika wa Seneti ya Burundi, Shimilimana Siliyake, alisema mashindano hayo yatumike kuhamasisha wakimbizi raia wa Burundi wanaohifadhiwa kwenye kambi za wakimbizi nchini Tanzania kurejea nchini Burundi kwa kuwa kwa sasa kuna amani.

"Ushirikiano huu ni njia ya wazi ya kuyadhihirishia mataifa mengine kuwa Burundi sasa ni shwari na raia wake wanapaswa kurejea nchini," alisema.

Kwa upande wa Ofisa Utamaduni Mkoa wa Kigoma, Revocatus Lutera, alisema tangu kuanza kwa michuano hiyo miaka minne iliyopita, lengo lililokusudiwa katika kuboresha ujirani mwema na masuala ya kiusalama limefanikiwa.

Alisema hiyo ni chachu kwa maeneo mengine yanayopakana na nchi zingine, kutumia njio hiyo katika kubuni vitu mbalimbali vya kufanya pamoja kama ilivyofanya Mkoa wa Kigoma.

# Michezo

Jumatatu Desemba 14, 2020

Nipashe




Lampard aitoa Chelsea ubingwa EPL UKURASA 22

# Simba sasa yaipangulia gia Yanga kileleni

## ●●● Yaanza kwa kuishusha Azam baada ya kuibuka...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na nahodha John Bocco, limeifanya Simba kuanza kupangua 'gia' za mbio za kuisaka Yanga kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya jana.

**Kwa ushindi huo, Simba ambayo bado ipo mechi mbili nyuma, sasa imekwea hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kufikisha pointi 29, ikiishusha Azam FC hadi nafasi ya tatu.**

Katika mechi hiyo, Simba ambayo ilianza na mastraika wawili mbele, iliandika bao hilo pekee dakika ya 32, baada ya Bocco kumegewa pande na kiungo mnyumbulifu na mbunifu, Clatous Chama, ambaye alikuwa na kazi ya kuwalisha mipira straika huyo na mwenzake, Meddie Kagere.

Baada ya kupewa pasi hiyo, mfungaji akawahadaa mabeki wa Mbeya City kama anautuliza, lakini hakufanya hivyo, badala yake aliupisha na yeye mwenyewe kugeuka kabla ya kuachia shuti lililomshinda kipa Lameck Kayonga na kujaa wavuni.

Kwa ushindi huo wa bao 1-0, Simba imekaa kwenye nafasi ya pili, ikisubiri mechi ya leo kwenye Uwanja wa Azam Complex kati ya wenyeji Azam FC dhidi ya Namungo FC.

Na ushindi kwa Azam tu yenye pointi 27 ndio utaweza kuiengua Simba kwenye nafasi ya pili, lakini kitendo cha kupoteza au sare kwa Azam itakuwa inaendelea kuwa kwenye nafasi ya tatu.

Kwenye mechi ya jana, iliwachukua Mbeya City sekunde 30 tu tangu mechi kuanza kulifikia lango la Simba, baada ya krosi ya Kibu Denis kuleta kizaazaa langoni, lakini mabeki walifanikiwa kuuondosha.

Shuti la mbali na Chama nusura liipe Simba bao dakika ya 20, lakini likagonga nguzo ya pembeni na kabla haujatinga wavuni, kipa Lameck Kayonga aliuwahi na kuudaka.

Kagere, alikosa bao kwa kushindwa kuunganisha krosi safi kutoka kwa Hassan Dilunga dakika ya 37.

Mbeya City ilipata nafasi safi ya kusawazisha bao dakika moja kabla ya mechi kwenda mapumziko, baada ya krosi ya Juma Shemvuni kumkuta Kibu aliyeisumbua mno beki wa Simba, aliyepiga kichwa kilichopaa langoni.

Kipindi cha pili, timu zote zilifanya mabadiliko, Simba ikimtoa Bocco na kuingia Chris Mugalu ambaye ni mechi yake ya kwanza baada ya muda mrefu wa majeruhi, lakini hakuwa kwenye wakati mzuri kutokana na viungo wa Simba kukamatwa na wale wa Mbeya City.

Lakini pia Dilunga alitoka na nafasi yake kuchukuliwa na Miraji Athumani, lakini hata hivyo hakufanya lolote la kuweza kubadili matokeo hayo, huku pia Erasto Nyoni akiingia badala ya Hamisi Ndemla.

Kipindi cha pili timu zote zilionekana kucheza mipira mirefu ya juu ambayo haikuwa na tija, huku mpira ukiwa hautulii.

Shambulizi hatari pekee kipindi chote cha pili lilikuwa ni dakika ya 72, wakati Josh Onyango na Ibrahim Ame walipotegeana kumdhibiti Kibu, ambaye aliudokoa kuelekea wavuni, kabla ya Onyango kuuondoa kwenye msitari, lakini wakati huo huo mwamuzi akisema kipa Aishi Manula alifanyiwa madhambi.

Simba sasa imecheza mechi 12, zikiwa ni mbili nyuma ya watani zake wa jadi Yanga, ambao wamecheza mechi 14, wakiongoza ligi kwa pointi 37.

**NDIYO ZANGU...**



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco, akimiliki mpira kwa kichwa dhidi ya mabeki wa Mbeya City kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara ambayo aliifungia timu yake bao pekee wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana. Anayesubiri kujibu mashambulizi pembeni ni Hamisi Ndemla. **MPIGAPICHA WETU**

# Okwi akutwa na corona Uganda

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA wa zamani wa Simba na Yanga, anayeichezea timu ya Al-Ittihad ya Ligi Kuu Misri sambamba na timu ya Taifa ya Uganda (Uganda Cranes), Emmanuel Okwi, amepata maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, imethibitishwa.

Okwi ambaye amelazimika kuendelea kubaki Uganda ili kujiweka karantini, ameukosa mchezo wa ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Misri 2020/21 ambao timu yake ya Al-Ittihad iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Pyramids FC juzi, Jumamosi.

Al-Ittihad ilieleza katika taarifa yake kuwa: "Kurejea kwa straika Mganda Emmanuel Okwi kumeahirishwa baada ya kupata maambukizi ya virusi vya corona."

"Matokeo ya vipimo vya virusi vya corona vilivyofanyika kwa mchezaji wa kimataifa wa Uganda, Emmanuel Okwi wa Klabu ya Al Ittihad ya Alexandria kabla ya kuondoka nchini kwao vimeonyesha kuwa amekutwa na maambukizi ya corona.

"Mchezaji alipata taarifa hizo za vipimo wakati akijiandaa kurejea Misri kuungana na timu kwa ajili ya maandalizi ya mechi (ya msimu mpya), lakini kukutwa huko na maambukizi kunamfanya sasa kusubiri hadi baadaye.

"Kutoka moyoni tunamtakia kupona haraka straika wetu Mganda Emmanuel."

Okwi aliondoka Misri mwaka huu baada ya kuibuka kwa virusi vya corona, lakini aliendelea kukwama Uganda kutokana na kufungwa kwa anga kwa kipindi kirefu sababu ikiwa ni kuzuia kuenea kwa virusi hivyo, lakini pia sababu nyingine ikiwa ni kukosekana kwa ndege za moja kwa moja kutoka Uganda hadi Misri.

Okwi anakuwa mchezaji wa pili Uganda Cranes kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona Misri baada ya Derrick Nsibambi aliyekuwa akiichezea Smouha ya huko kukutwa na maambukizi Julai, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >